# USAWIRI WA VIPENGELE VYA KIUHALISIA KATIKA FASIHI YA WATOTO: MFANO WA RIWAYA YA *KIJANA MPELELEZI*, WAMITILA K. W (2007) NA *USIKU WA MANANE*, KOBIA J. (2010)

**ROSE NDANU MBOYA**

**Tasnifu Hii Imetolewa Ili Kutosheleza Baadhi Ya Mahitaji Ya Shahada ya Uzamili Katika Chuo Kikuu Cha South Eastern Kenya**

**2024**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi:……………………………………… Tarehe:…………………………

Rose Ndanu Mboya

C410/KIT/20001/2018

(Mtahiniwa)

Tumeidhinisha kutolewa kwa tasnifu hii kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha South Eastern Kenya kwa ajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili.

Sahihi:……………………………………… Tarehe:…………………………

Dr. Chomba Esther

Msimamizi

Sahihi:……………………………………… Tarehe:…………………………

Dr. F. Mwangangi Musyoka

Msimamizi

## SHUKURANI

Sina budi kuwashukuru watu wote waliochangia katika ufanisi wa tasnifu hii. Hata ingawa ni vingumu kuwataja wote, Siwezi kusahau kuwataja baadhi yao ambao bila shaka msaada wao ungekosekana, tasnifu hii haingekamilika vilivyo.

Mwanzoni shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Daktari Esther Chomba na Daktari Francis Mwangangi Musyoka kwa jinsi ambavyo walikuwa tayari kunihudumia kila mara nilipowaendea kutaka msaada. Walinifungua macho na kunionyesha jinsi ya kushughulikia suala la utafiti kitaalamu. Usaidizi wao umenifaa katika kuandika kiusomi na kwa kujiamini.

Aidha, nawajibika kuwashukuru wahadhiri wote walionifundisha katika kozi hii ya uzamili na kunipa ushauri katika vikao vya mawasilisho na michango kwa njia mbalimbali katika hatua za kukamilisha tasnifu hii. Hao ni Daktari Kaui, Daktari Kamau na Daktari Sarah Ngesu na Daktari Janet Mulwa. Tasnifu hii isingekamilika bila mafunzo na ushauri wao. Asanteni nyote kwa kunivumilia na kunielekeza.

Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu wote tuliosoma pamoja na kutiana shime kama vile akina Mercy Mwendwa, Christmas Nyamai na Rhoda.Nyote niliowataja na wale ambao sikuweza kuwataja, Mungu awabariki.

## TABARUKU

Kwa mume wangu Joseph Mboya, Watoto wetu Gladys, Jackson, Tom, Mumbe, Gloria, Virginia na wajukuu zangu Amani na Josephlogan. Jitahidini katika usomi kwani elimu ni nguvu maishani.

## YALIYOMO

**Ungamo** ........ ii
**Shukurani** ........ iii
**Tabaruku** ........ iv
**Yaliyomo** ........ v
**Viambatisho** ........ vii
**Akronimu na Vifupisho** ........ viii
**Ufasili wa Dhana Muhimu** ........ ix
**Ikisiri…** ........ x

**SURA YA KWANZA**

**1.0 Utangulizi** ........ 1
1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Usuli wa Mada ........ 1
1.3 Suala la Utafiti ........ 6
1.4 Madhumuni ya Utafiti ........ 6
1.5 Maswali ya Utafiti ........ 6
1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 7
1.7 Upeo na Mipaka ........ 8

**SURA YA PILI**

**2.0 Mwauo wa Machapisho** ........ 9
2.1 Utangulizi ........ 9
2.2 Uhusika katika Fasihi ya Watoto ........ 9
2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 13
2.4 Msingi wa Nadharia ........ 18
2.4.1 Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa ........ 19
2.4.2 Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ........ 21

## SURA YA TATU

**3.0 Mbinu za Utafiti** ........ 23
3.1 Utangulizi ........ 23
3.2 Muundo wa Utafiti ........ 23
3.3 Eneo la Utafiti ........ 23
3.4 Kikundi Lengwa ........ 24
3.5 Uteuzi wa Sampuli ........ 24
3.6 Ukusanyaji wa Data ........ 25
3.7 Uchanganuzi wa Data ........ 25
3.8 Maadili ya Utafiti ........ 25
3.9 Hitimisho ........ 25

## SURA YA NNE

**4.0 Uchanganuzi wa Data na Matokeo** ........ 27
4.1 Utangulizi ........ 27
4.1.1 Maudhui ya Siasa ........ 27
4.1.2 Maudhui ya Vitisho ........ 33
4.1.3 Maudhui ya Vita ........ 35
4.1.4 Maudhui kuhusu Usalama wa Kitaifa ........ 37
4.2 Usawiri wa Wahusika Watoto ........ 40
4.2.1 Mtoto Kupewa Majukumu ya Kiupelelezi ........ 40
4.2.2 Mtoto Kusawiriwa kama Jasiri ........ 41
4.2.3 Usawiri wa Jinsia Katika Maudhui ya Usalama ........ 44

## SURA YA TANO

**5.0 Hitimisho na Mapendekezo** ........ 46
5.1 Utangulizi ........ 46
5.2 Muhtasari ........ 46
5.3 Mapendekezo ya Utafiti ........ 47
**Marejeleo ........ 51**

## VIAMBATISHO


Kiambatisho A: A childs exposure to violence can lead to lasting physical, mental and emotional harm. Georgina Cranston/Reuters……………………………………………………56

Kiambatisho B: Watoto Kuangamia Katika Vurugu Baada Ya Uchaguzi Mkuu. (Stephanie Moraa kutoka Mathare, Nairobi na Baby Samantha Pendo Kutoka Kisumu)…………………………………………...…..57

Kiambatisho C: Daily Nation July 25, 2018……………………………………….58

Kiambatisho D: Utaratibu wa kazi……………………………………………………59

Kiambatisho E: Makadirio ya gharama ya utafiti………………………………….60

## AKRONIMU NA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **BBI** | **:** | Buiding Bridges Initiative |
| **EAEP** | **:** | East African Educational Publishers |
| **ECK** | **:** | Electoral Commission of Kenya |
| **IEBC** | **:** | Independent Electoral and Boundaries |
| **ICJ** | **:** | International Court of Justice |
| **JKF** | **:** | Jomo Kenyatta Foundation |
| **KICD** | **:** | Kenya Institute of Curriculum Development |
| **KLB** | **:** | Kenya Literature Bureau |
| **KTN** | **:** | Kenya Television Network |
| **Mh** | **:** | Mhariri |
| **OUP** | **:** | Oxford University Press |
| **PNU** | **:** | Party of National Unity |
| **WH** | **:** | Wahariri |

## UFASILI WA DHANA MUHIMU

**Maudhui:** Ni masuala yanayorejelea mambo ambayo yamezuka katika jamii na yanayoiathiri moja kwa moja. Ni masuala yanayoangaziwa sana na waandishi wa kazi za fasihi yoyte ile.

**Fasihi ya Watoto:** Ni Sanaa inayotumia lugha kwa ubunifu ili kuwasilisha ujumbe unaolenga watoto kama hadhira yake.

**Hadithi za Watoto:** Kwa mujibu wa utafiti za watoto ni masimulizi yanayochapishwa kwa kusudi la kusomwa na watoto hasa walio katika shule za msingi gredi nne hadi la nane.

**Watoto:** Fasiri ya kikatiba nchini Kenya inatambua watoto kama watu walio na umri wa chini ya miaka kumi na minane. Katika tasnifu hii, istilahi hii hasa inarejelea watoto kuwa wasichana na wavulana kati ya miaka tisa na kumi na mitatu ambao wako katika shule za msingi gredi la nne hadi la nane. Hawa ndio hasa walengwa wa hadithi za watoto zinazorejelwa katika utafiti huu.

**Uhalisia:** Istilahi inayorejelea kimsingi mtindo wa uandishi unaojishughulisha na utoaji wa taswira ya maisha ya kawaida katika jamii mahususi.

**Usalama:** Hali ya kutokuwepo hatari au fujo.

# IKISIRI

Mada ya utafiti huu ni kuchunguza uhalisia wa maudhui ya usalama katika fasihi ya watoto mfano wa riwaya *ya Kijana Mpelelezi (Wamitila, K.W.2007)* na *Usiku wa Manane (Kobia, J 2010)*. Hadithi hizi za watoto zimejikita katika fasihi ya watoto. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kutathmini uhalisia wa maudhui yanayohusu usalama na yanayonuiwa watoto kama hadhira lengwa, kubainisha maudhui ya usalama yaliyodhihirishwa na waandishi na kueleza jinsi wahusika watoto wanaohusishwa na maudhui ya usalama wanavyosawiriwa na waandishi wa riwaya teule. Nadharia za Uhalisia wa kijamaa na Soshiolojia ya fasihi zilizotumiwa katika utafiti huu zilitoa msingi madhubuti kuwa maswala ya usalama yanayobainika yanafungamana na hali ilivyo katika maisha ya jamii ya karne hii ya ishirini na moja. Vita vya kikabila na ukosefu wa usalama katika jamii yapaswa kuondolewa na kusahaulika kabisa. Hadithi za watoto za waandishi hawa ziliteuliwa kimakusudi kwa kutumia sampuli lengwa kutokana na upekee wa kimaudhui uliodhihirisha uhalisia. Hadithi zilizoteuliwa zilisomwa, data kuhusu uhalisia wa maudhui ya usalama kwa mujibu wa maswali ya utafiti zilioneshwa. Data iliyopatikana kuhusu maudhui ya usalama katika kila hadithi ilichanganuliwa. Mwisho, matokeo na mapendekezo ya utafiti yaliwasilishwa kimaelezo. Matokeo yalionesha kuwa siasa za kikabila zinazoenezwa katika nchi hii kipindi baada ya kipindi, vitisho vinavyoleta migogoro katika jamii na maudhui mengine mengi yanayosababisha ukosefu wa usalama ni hatari kwa vizazi na vizazi na kuna haja ya kuchukua hatua za dharura kuwafahamisha watoto kupitia hata maandishi kuhusu umuhimu wa amani katika taifa ili wakikua wawe na uwezo wa kueneza maridhiano baina ya makabila yote. Utafiti huu unatarajiwa kuwa muhimu kwa wasomi na waandishi wa fasihi ya watoto. Utafiti huu unaongeza maarifa katika uhakiki wa hadithi za watoto kwa kuangazia mielekeo ya uhalisia wa kimaudhui ya usalama katika jamii. Mwishowe, tumetoa pendekezo la utafiti zaidi.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Utangulizi

Wamitila, K.W (2008) anasisitiza kuwa utanzu wa fasihi ya watoto umepuuzwa kwa kipindi kirefu miongoni mwa maandishi ya kihakiki. Fasihi ya watu wazima imeshughulikiwa sana kihakiki labda hii ni kwa sababu ya imani ya kuwa fasihi ya watoto haifai kuhakikiwa kinadharia au kwa kuwa inahusu tu ngano kama za fasihi simulizi. Utafiti huu unakusudiwa kuchangia kuziba pengo kwamba maswala ya usalama yakishindiliwa akilini mwa watoto, miaka ijayo amani itadumishwa.

Katika utafiti huu, tulichunguza fasihi ya watoto ambayo inawasilishwa kwa njia ya hadithi za watoto. Hadithi hizi za watoto zinadhihirika kutokana na kuwa, wahusika wakuu ni watoto, lugha ni nyepesi na msamiati uliteuliwa kwa makini. Pia mwandishi alihakikisha kuwa lengo kuu ni kuwaadilisha watoto. Hadithi hizi zimetumiwa kuweka wazi mawazo ya mwandishi kuhusu jamii. Mwandishi huiendeleza kazi yake kwa mtazamo wa mtoto na kuhakikisha kuwa inafungamana na matarajio na matamanio ya hadhira ya watoto. Watoto aghalabu huyaona mambo kwa mtazamo tofauti na watu wazima.

### 1.2 Usuli wa Mada

Fasihi ya watoto huongozwa kwa kiasi kikubwa na maoni au mawazo kama yalivyo katika jamii kuwahusu watoto. Mtazamo huu unaathiri kwa kiasi kikubwa jinsi tunavyoteua kazi za fasihi pamoja na matarajio tuliyonayo kuhusu kazi za fasihi ya watoto. Hii inahusiana na kuandikwa kwa kazi hizo, maudhui yake, wahusika wake na mwelekeo wake. Hivyo, fasihi ya watoto huongozwa na mtazamo wa jamii kutokana na ukweli kuwa waandishi wengi wa fasihi ya watoto ni watu wazima na wala si watoto wenyewe.

Mojawapo wa nyanja muhimu za fasihi andishi ni fasihi ya watoto. Tanzu za fasihi andishi ni kama vile riwaya, tamthilia, ushairi, hadithi fupi na novella. Fasihi ya watoto hususan hutumia wahusika kama vile wanyama, mazimwi na binadamu ili kuweza kupendeza hadhira yake. Kulingana na Wamitila, (2003) fasihi ya watoto huandikwa kwa ajili ya

kusomwa na watoto. Fasihi ya watoto aghalabu hupitishwa kwa wasomaji na kuhifadhiwa kama hadithi za watoto zilizochapishwa.

Hata hivyo zipo tanzu ambazo zimeandikwa kwa mitindo tofauti kama vile ushairi na tamthilia. Ushairi ambao umeandikwa ili kusomwa na watoto wadogo huwa mwepesi, haujakuzwa na kuendelezwa sana. Tamthilia ambazo zimeandikwa ili kusomwa na watoto nazo huwa nyepesi kimaelezo na katika muundo na huzingatia kanuni za kimsingi tu. Baadhi ya tamthilia hizo zinatokana na hadithi zinazosimuliwa kama vile *Kifimbo cha Cheza* (Ahmed, 2003) na *Kesi ya Kuchekesha* (Wamitila, 2006)

Fasihi ya watoto pia inaweza kusheheni vitabu vya picha. Nyingi za kazi za fasihi ya watoto huwa za kuadilisha, yaani kukuza, kujulisha na kuendeleza maadili au mafunzo fulani. Lengo hili hupatikana kupitia kwa maudhui na fani ya kazi zenyewe. Ngugi (2009) anaeleza kuwa kazi ya fasihi ya watoto ni tofauti kulingana na mataifa mbalimbali. Anaeleza kuwa katika nchi nyingi za kimagharibi kwa mfano, fasihi ya watoto imeendelea zaidi kuliko ilivyo katika mataifa ya Kiafrika. Asilimia kubwa ya watoto katika mataifa hayo ina elimu na kuwawezesha kusoma fasihi iliyoandikwa. Kenya miongoni mwa nchi nyingi za Afrika, ina ukuaji wa fasihi ya watoto ambao umepitia mikondo mingi ili kufikia ilipo sasa. Kairu (2005) anasema kuwa katika kipindi cha kabla ya ukoloni fasihi ya watoto ilikuwa simulizi. Fasihi hii ilitokana na tajiriba za watu katika maisha na jinsi walivyohusiana pamoja na maingiliano katika jamii walipoishi. Watoto walipata picha halisi ya jamii zao na falsafa yao. Kutokana na hadithi hizi watoto walifunzwa maadili na kukashifu tabia mbaya kama vile ulafi, uchafu, ukatili na kuelezwa athari zake.

Katika kipindi cha ukoloni, fasihi ya watoto iliandikwa na wakoloni waliokuwa wazungu. Kairu (2005) akimrejelea Mpesha (1996) anasema kuwa kipindi hicho cha ukoloni kilibadilisha fasihi iliyosomwa na watoto shuleni. Fasihi iliyoandikwa na kusomwa shuleni ilihusishwa na utamaduni wa kigeni. Fasihi hii pia ilidunisha ile ya kiafrika na kuipuuza. Nia yake ilikuwa kumchora mwafrika kama mtu duni aliyeishi kama hayawani na aliyekosa maendeleo yoyote yale. Nia yake ilikuwa kumdanganya mwafrika kuwa utamaduni wake ulikuwa usiofaa.

Mwishoni mwa kipindi cha ukoloni, waandishi wa kiafrika waliandika hadithi za watoto ambazo zilisomwa shuleni. Hadithi za kipindi hiki zilifanya kila jitihada kuinua hadhi ya mwafrika kupitia mitazamo ya kiafrika. Mifano michache hizo ni hadithi *ya Adili Na Nduguze* (shaaban, 1952*)*, *Lila na Fila* (Kiimbila, 1966) *na Kurwa na Doto* (Farsy, 1960) Baada ya ukoloni fasihi ya watoto ilijaribu kubadilisha mafunzo ya kikoloni kuhusu mwafrika kuwa mtu duni. Ilitilia mkazo maslahi ya mtoto wa kiafrika na uzoefu wake. Baadhi ya vitabu vya watoto vilivyopendekezwa kutumiwa shuleni vilikuwa pamoja na *Kaka Sungura na Wenzake* (Nelson Publisher, Kenya.1966), *Nani Mjinga?* (Michuki, 1967) na *Hadithi za Furaha* (Kitula King'ei,1989)

Jambo linalodhihirika kuhusiana na historia hii ni kuwa fasihi ya watoto imezidi kuonesha mitazamo ya kijamii na hali yake ya kimaisha katika jamii. Katika karne ya ishirini kwa mfano, hadithi nyingi zilimwonesha mtoto wa kiume kuwa shujaa. Hii ni kutokana na mitazamo ya ubabedume kama anavyosema Howe (1970) katika makala yake kuhusu yanayotarajiwa kutokana na jinsia yao. Kwa mfano, waliambiwa kuwa wavulana hawalii kwa kuwa wanapaswa kuwa jasiri lakini wasichana hulia kwa kuwa ni wanyonge na wenye hisia dhaifu. Waliowafunza watoto mitazamo hii ni watu waliotangamana nao katika maisha wakiwemo wazazi wao, walimu, walimu wa dini na hata watoto wenzao. Wanajamii walichukua mawazo haya na yakakwama akilini mwao. Mawazo kama haya yalionekana wazi katika vitabu vya hadithi vyenye wahusika wakuu ambao ni watoto wa kiume vya karne iliyopita. Kwa mfano, hadithi ya *Tajiri Mjanja* (Omolo, 1967*)*, *Bonde la wafu* (Manji, 1996*)*, *Atendaye mema* (Mailu, 1997) *na Androko na Simba* (Mkufya,1998).

Nchini Kenya, fasihi ya watoto imepata umaarufu kufikia miaka ya 2000 baada ya kujumuishwa katika somo la Kiswahili kuanzia shule za msingi hadi sekondari. Vile vile, hatua ya serikali ya kugharamia masomo imechangia pakubwa katika maendeleo haya kwa sababu serikali ilichukua jukumu la kununua vitabu vya ziada na vya kiada.

Katika Karne ya ishirini na moja uandishi wa hadithi za watoto katika lugha ya Kiswahili umefana sana kimaudhui. Kukua huku kunadhibitika kutokana na kuandikwa idadi kubwa ya vitabu vya hadithi za watoto vinavyochapishwa na wachapishaji mbalimbali.

Waandishi wengi wa hadithi za watoto ni maarufu katika fasihi ya Kiswahili kwa jumla na wana tajiriba kubwa ya Kiswahili. Wengi wa waandishi walio mashuhuri ni wahadhiri katika vyuo vikuu, walimu katika shule mbalimbali na wengine ni wasomi walio na vipaji vya kuandika kazi za fasihi.

Usomaji wa hadithi za watoto ulipiga hatua baada ya Kiswahili kilipofanywa kuwa somo la lazima katika shule za msingi mwaka 1985 na hata ukazidi kuimarika baada ya kuanzishwa mfumo wa elimu bila malipo katika shule za msingi nchini mwaka wa 2003. Ngugi (2009) akimnukuu Mbaabu (1996) anasema kuwa baada ya mfumo wa 8-4-4 kuanzishwa vitabu vya fasihi ya watoto vilianza kuchapishwa kwa wingi. Hii ni kwa kuwa Kiswahili kilifanywa kuwa somo la lazima na linalotahiniwa katika shule za msingi na hivyo basi vitabu vya hadithi za Kiswahili vikahitajika zaidi.

Elimu bila malipo katika shule za msingi ilipoanzishwa, iliwafanya wanafunzi wengi kusoma vitabu vya hadithi za watoto kwa kuwa shule zilipewa pesa na serikali za kununulia vitabu vikiwemo vitabu vya hadithi Ngugi (2009).Kwa mujibu wa Miricho (2015), Uchapishaji wa hadithi za watoto ulipigwa jeki shule zilipoanza kununua vitabu vya hadithi kwa wingi kuliko hapo awali. Wachapishaji wengi walianzisha miradi ya kuchapisha vitabu vya fasihi ya watoto kwa wingi ili kutosheleza mahitaji ya shule. Wizara ya Elimu (2015), ilitambua wachapishaji wengi kwa mfano *Jomo Kenyatta Foundation* ambao walianza kuchapisha mfululizo wa hadithi za *Adili, Kenya Literature Bureau* ambalo lilianza mfululizo wa hadithi za *Nasaha zetu, Phoenix, OUP, Sasa Sema (Longhorn), EAEP, Moran, Vide-muwa*. Ukuaji na uenezaji wa fasihi ya watoto umechangiwa kwa pakubwa na Mashirika haya ya uchapishaji.

Miaka ya hivi karibuni, ubora wa vitabu vya fasihi ya watoto vinavyochapishwa umeimarika. Ngugi (2009) anasema kuwa ubora huu umechangiwa na Taasisi ya ukuzaji mitaala (KICD) kwa kuwa inakagua iwapo vitabu vinavyochapishwa vinafaa na kuidhinisha vile vinavyofaa kusomwa na watoto shuleni. Jambo hili linafanya waandishi na wachapishaji kujitahidi kutimiza viwango vya ubora vinavyowekwa na taasisi hiyo. Pia kumekuwa na mashindano mbalimbali ya waandishi kung'ang'ania zawadi ambazo

zinawahamasisha kuandika hadithi bora za watoto. Mashindano kama hayo ni Tuzo ya fasihi ya Jomo Kenyatta na Tuzo ya uandishi ya Wahome Mutahi.

Usomaji wa fasihi ya watoto unaweza kumwathiri mtoto kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kobia, (2010) anaweka haya wazi kwa kutoa maoni kuwa watoto wakifunzwa masuala ya amani na kuweka ujirani vivyo hivyo kufikia utu uzima uhasama hautakuwepo. Matundura (2007) anaeleza kuwa fasihi ya watoto husomwa katika kipindi ambacho watoto ni wachanga na wanapokua huamini kuwa mambo mengi wanayosoma kuwa ndiyo ukweli wa maisha. Hii ni kwa kuwa hawawezi kubainisha ni yapi ya kufuata na ni yapi ya kutupilia mbali. Kwa mujibu wa Miricho, (2015), ina maana kuwa waandishi huzingatia vilivyo taswira za watoto zinazojitokeza katika hadithi wanazotunga ili zinaposomwa na watoto ziweze kuwasilisha taswira zifaazo kwa hadhira lengwa.

Utafiti huu uliangazia maudhui ya usalama katika fasihi ya watoto nchini Kenya. Mtafiti aliteua vitabu vya miaka ya karne hii ya ishirini na moja kwa utafiti huu. Vitabu hivyo ni *Usiku wa Manane* cha Kobia, J (2010) kilichochapishwa na Kenya Literature Bureau Nairobi na *Kijana Mpelelezi* kilichoandikwa na Wamitila, K.W (2007) na kuchapishwa na Vide-Muwa Publishers Limited. Njogu na Chimerah, (1999) wanatoa usemi kuwa mwandishi hawezi kuandika kando ya mambo yanayoendelea katika jamii yake kwa sababu anaelewa jamii yake. Kutokana na sababu hii tunaona kuwa Kobia, (2010) na Wamitila, (2003) ambao ni wasomi na wakenya bila shaka wanaelewa sababu za ukosefu wa usalama nchini Kenya kipindi baada ya kipindi. Athari kama hizi ziliweza kuchochea uandishi wao wa hadithi kama vile *Usiku wa Manane (Kobia, 2010)* na *Kijana Mpelelezi (Wamitila, 2007).*

Ukweli wa kauli hii ulibainika katika utafiti huu uliotumia nadharia ya Uhalisia wa kijamaa na Sosholojia ya fasihi kwa kujaribu kuonesha kuwa yanayoandikwa katika fasihi ya watoto ni mfano wa jinsi maisha ya jamii halisi yalivyo ijapokuwa yametengenezwa na kuwa ya ulimwengu wa kubuni kulingana na mwandishi.

### 1.3 Suala la Utafiti

Tasnifu nyingi za fasihi ya watoto zimeweza kufanywa, lakini utafiti wa kina kuhusu maswala ya usalama na jinsi yakitomewa katika bongo za watoto wakiwa bado wachanga nchi inavyoweza kupata amani ya kudumu bado haujafanywa.

Uhalisia katika jamii unaonyesha kwamba watoto huathirika katika kukua kwao kutokana na sifa za wahusika wanaowapenda. Wao huamini masuala mengi wanayoyapitia wahusika wanaowasoma kuwa ni kweli. Nyingi za hadithi za watoto huwa na wahusika wanyama na mazimwi hasa ikiwa zimechota visa vya fasihi simulizi. Mazimwi na wanyama huweka wazi maudhui kwa hadhira ya watoto wanaozisoma kazi hizo, lakini kazi zinazotumia wahusika ambao ni binadamu zinaweza kuwa na athari kubwa mno kwa mtoto msomaji kwa kuwa matendo ya wahusika hao yanakaribia uhalisia wa binadamu katika maisha ya kila siku.

Utafiti huu ulilenga kuziba pengo hili kwa kuchunguza maswala yanayopelekea ukosefu wa amani katika hadithi ya *Usiku wa Manane, Kobia* (2010) na *Kijana Mpelelezi, Wamitila,* (2007).

### 1.4 Madhumuni ya utafiti

i. Kubainisha maudhui ya usalama yaliyodhihirishwa na waandishi wa riwaya za *Usiku wa Manane (Kobia*, 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007).
ii. Kueleza jinsi wahusika watoto wanaohusishwa na maudhui ya kiusalama wanavyosawiriwa katika hadithi za *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007).
iii. Kutathmini uhalisia wa maudhui yanayohusu usalama na yanayonuiwa watoto kama hadhira lengwa katika riwaya za *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007).

### 1.5 Maswali ya utafiti

i. Je, ni maudhui gani ya kiusalama yanayojitokeza katika hadithi ya *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007)?

ii. Je, wahusika watoto wanaohusishwa na maudhui ya usalama wamesawiriwa vipi katika riwaya za *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007)?

iii. Je, ni vipi maudhui ya kiusalama katika riwaya za *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007) yanadhihirisha uhalisia wa kijamii katika kipindi husika.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Usawiri wa wahusika watoto katika hadithi huathiri mielekeo ya watoto halisi wanaosoma hadithi katika kukua kwao. Aidha watoto wakiwa na mazoea ya kusoma vitabu vinavyorejelea masuala ya amani watapata nafasi ya kufaidika kimaadili na athari yake itabainika kupitia kwa udumishaji wa amani na maridhiano. Yakiwaathiri watoto wenzao ifaavyo, watoto wengi watapata ilhamu ya kusoma. Hiki pia kitakuwa kichocheo kikubwa kwa waandishi na wachapishaji. Jambo hili hatimaye litasaidia kupalilia maadili miongoni mwa wanajamii na kujenga mazoea ya kuweka amani miongoni mwa watoto na nchi kwa jumla. Maeneo yanayokumbwa na ukosefu wa usalama hupata shida zinazorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, hivyo wakisoma masuala haya mapema wataweka amani na maridhiano miongoni mwao.

Utafiti huu pia unatarajiwa kuwafaa wachapishaji katika mikakati ya kukuza sera zao za uchapishaji wa vitabu vya fasihi ya watoto ili kuendelea kuimarisha ubora wa vitabu vinavyochapishwa vya fasihi ya watoto. Utafiti huu utawawezesha wapanga mitaala na waundaji sera za elimu kupata vigezo watakavyotumia katika uteuzi wa vitabu vinavyofaa katika viwango tofauti vya elimu. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa mchango muhimu katika taaluma ya fasihi ya watoto. Matokeo yake yataongeza maarifa kuhusu uhakiki wa hadithi za watoto hasa kwa kuangazia mielekeo mipya ya kimaudhui inayohusishwa na watoto. Matokeo ya utafiti huu basi yatakuwa muhimu kwa wasomi, waandishi na wachapishaji wa fasihi ya watoto.

Utafiti huu utakuwa muhimu pia katika ufundishaji wa fasihi ya watoto hasa kuhusiana na suala la uhalisia wa maudhui katika fasihi ya watoto na kuhusu nadharia ya uhalisia wa

kijamaa. Utafiti huu utakuwa wa thamani kwa watoto kwa kuwa utatoa mapendekezo muhimu ya tafiti za baadaye. Aidha, matokeo ya utafiti huu yatakuwa muhimu katika kuangazia dhima ya hadithi za watoto kama wenzo wa maarifa ambayo yatawezesha kuelewa mivutano ya kisiasa nchini mwao kwa nia ya kuhubiri na kufunza amani kama inavyotakiwa katika hali halisi ya kijamii. Mathalani viongozi wa taifa nchini Kenya walikuwa wanazua mabadiliko ya kikatiba (BBI) ili kumaliza migogoro ya kisiasa katika taifa.

**1.7 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulichunguza maudhui ya kiusalama na jinsi yanavyohusishwa na watoto katika jamii na katika hadithi za *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007).Kazi hizi ziliteuliwa kwa kuwa utafiti awali ulibainisha kuwa waandishi wa riwaya hizi waliwatumia watoto kama wahusika katika kazi zao. Pia ni hadithi ambazo zinawalenga watoto wa gredi ya nne hadi ya nane. Utafiti huu unahusu uhalisia wa maudhui ya usalama katika fasihi ya watoto. Mtafiti alichanganua magazeti ya *Standard, Nation na Taifa Leo* yaliyotangaza matukio yaliyojiri nyakati za fujo baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya.Pia runinga za Citizen, KTN News, Deutche Welle World News zilizopeperusha habari kuhusu masuala ya kiusalama hasa yanayowahusu watoto ili kuonesha uhalisia uliopo kati ya fasihi za watoto na jamii husika. Mwaka wa 2017 Samantha Pendo mtoto wa takriban miezi sita kutoka Kisumu na Stephanie Moraa msichana wa miaka nane waliuawa kutokana na ghasia hizi. Katika maudhui utafiti huu ulichunguza ni nini watoto wanaambiwa kuhusu siasa, vitisho, vita na usalama wa kitaifa ili kuona kama yanayozungumziwa katika riwaya husika hulandana na hali halisi.

## SURA YA PILI

## 2.0 MWAUO WA MACHAPISHO

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo kuhusu mapitio ya maandishi na misingi ya nadharia. Imetalii mawazo yaliyotokana na utafiti uliofanywa kuhusiana na fasihi ya watoto katika fasihi ya Kiswahili. Cha mno ni kuangazia uhusiano wa tafiti husika na utafiti huu ili kuonesha jinsi zilivyoufaa utafiti huu wa sasa. Baadhi ya maandishi na tafiti zinazohusu maudhui, fani na mikakati ya kiufundi katika fasihi ya watoto yameelezewa ili kubainisha pengo la kiusomi ambalo utafiti huu ulikusudia kuziba.

### 2.2 Uhusika katika fasihi ya Watoto

Hadithi za watoto hupatikana katika kitengo cha fasihi ya watoto. Ni hadithi ambazo ziliandikwa ili walengwa wake wakuu ambao watazisoma wawe ni watoto. Hadhira lengwa ya hadithi hizi ni watoto wa shule za msingi. Hadithi hizi za watoto, kama fasihi ya watoto ilivyo, huweza kuoneshwa kutokana na sifa fulani. Baadhi ya sifa hizo ni kama zifuatazo; -Watoto huwa ndio wahusika wakuu katika hadithi hizo. Wamitila (2008) anaeleza wahusika kuwa viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Wahusika huwa na sifa kadha za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa na ambazo hutambulishwa na yale wanayoyanena na kutenda.

Hadithi za watoto zinaweza kuwa na wahusika wa aina mbalimbali kama vile wanyama na hata watu wazima. Wahusika watu wakiwa wazazi au walimu wa watoto husika, lakini wahusika wakuu aghalabu huwa ni watoto. Hali hii hufanya fasihi iweze kushawishi mtoto aweze kuisoma kwa kuwa atatamani kujihusisha na mhusika huyo anayetajwa katika hadithi nzima hasa ikiwa mhusika yule ni shujaa na mwenye maadili mema. Iwapo ni wahusika wanyama waliotumiwa, wao huonyeshwa wakiiga vitendo vya watoto au vya watu ambao watoto huingiliana nao katika mazingira ya kila siku. Katika utafiti huu tulizingatia hadithi zilizo na mchanganyiko wa wahusika watoto na watu wazima ili kupata maudhui ya usalama. Kwa mfano, Kangwana, Maria, shangazi yao na mzee Majungu

katika *Kijana Mpelelezi (Wamitila 2007)*, Msimulizi, mamake na abiria waliosafiri pamoja katika hadithi ya *Usiku wa Manane (Kobia 2010)*.

Kuwepo kwa wahusika wakuu watoto kunapelekea mtazamo unaoihusu kazi inayoshughulikiwa kuwa ule wa watoto. Sifa hii hufanya kazi ya fasihi kuwavutia wasomi na kutaka kujilinganisha na wahusika wa hadithi hiyo. Hadithi za watoto mara nyingi huwa na mhusika aliye mwema na mwingine ambaye ni mbaya ili watoto waweze kupata mwanga wa linalokusudiwa. Kwa mfano katika hadithi ya kijana mpelelezi mzee Majungu amechorwa kama mhusika mwovu na uovu wake unafichuliwa na upelelezi wa Kangwana. Katika mfano huu watoto wanaosoma hadithi hii wataona wema ukishinda ubaya na hapo kuelekezwa vema kimaadili.

Hadithi za watoto huwa fupi na huonesha matendo. Hadithi ambayo ni ndefu itawachosha watoto wanaposoma na watakosa hamu ya kuisoma na kuimaliza. Hadithi zilizoteuliwa katika utafiti huu zina kurasa chache kati ya hamsini na sabini hivyo kuwafaa watoto.

Lugha inayotumika katika hadithi za watoto huwa rahisi kulingana na kiwango cha uelewa wa watoto wanaolengwa ili waweze kuifuata hadithi, kuifurahia na kupata ujumbe wake. Kwa mfano, hadithi zinazolenga watoto wa madarasa ya chini hasa darasa la nne na tano katika shule za msingi zina lugha nyepesi kuliko vitabu vya hadithi zinazolenga watoto wa madarasa ya sita, saba na nane. Sentensi zake mara nyingi huwa fupi na zenye miundo sahihi ili ujumbe uweze kung’amuliwa kwa urahisi na bila utata kwa kuwa urazini wa wasomaji chipukizi huwa wa kiwango cha chini. Msamiati wake huwa mwepesi unaolingana na kiwango cha watoto wanaolengwa. Maneno mapya hukolezwa rangi ili kuonekana kwa urahisi.

Picha tofauti za kuvutia na michoro ya kupendeza aghalabu yenye rangi mwafaka ni sifa nyingine katika hadithi za watoto. Picha hizi huvutia watoto ili kusoma hadithi, husaidia weledi wao, huwawezesha kukumbuka hadithi waliyoisoma na pia huipatia hadithi uhalisia. Picha na michoro ni njia mwafaka ya kupitisha ujumbe katika hadithi za watoto. Picha huwa zinaelekeza ujumbe unaowasilishwa na mwandishi mathalani, picha katika

hadithi ya *Kijana Mpelelezi* (Wamitila 2007) zinamsawiri Kangwana kama mvulana jasiri, asiyeogopa giza na anayejitokeza kuchungulia dirishani na kufanya upelelezi hata baada ya kusikia sauti za kushtua.

Maandishi ya hadithi za watoto huwa na ukubwa wa hati unaolingana na kiwango cha watoto wanaotazamiwa kusoma, kazi za watoto wa madarasa ya chini shuleni, ambao ndio wanaanza kujifunza kusoma, huwa na maandishi makubwa sana ili mtoto aweze kutambua herufi kwa urahisi na kuweza kusoma. Hadithi zinazopaswa kusomwa na watoto wa madarasa ya kati pia huwa na maandishi makubwa kiasi huku za watoto wa madarasa ya juu katika shule za msingi yakiwa na hati ndogo. Kwa mfano, kitabu cha *Usiku wa Manane (*Kobia 2010) na *Kijana Mpelelezi (*Wamitila *2007)* ambavyo vinakusudiwa watoto wa kuanzia darasa la sita vina maandishi madogo kiasi kuliko vya watoto wa chini ya darasa la sita.

Mtiririko wa hadithi za watoto huwa mwepesi na wa moja kwa moja. Kwa mfano, mbinu rejeshi au kisengerenyuma haitumiwi ili wasomaji wa umri mdogo waweze kufuata kisa moja kwa moja na kwa wepesi kutoka mwanzo, kilele hadi mwisho. Sifa hizi humwezesha mtoto msomaji kufuata matukio yote na kuelewa bila kuchanganyikiwa na tukio lolote. Kitabu kinachofaa cha kusomwa na mtoto ni kile ambacho mwandishi amefaulu kuwasilisha ujumbe moja kwa moja hadi kwa mtoto mwenyewe. Katika hadithi za utafiti huu mtiririko ni wa moja kwa moja kwa kuwa mwandishi ametumia mpangilio wa matukio, kilichosababisha matukio hayo na matokeo yake katika hadithi zote mbili.

Maudhui yanayopitishwa katika hadithi za watoto huwalenga watoto wenyewe. Wamitila (2008) anaeleza maudhui kuwa jumla ya masuala na mambo yanayojadiliwa katika kazi ya kifasihi. Waandishi wa hadithi za watoto huzama katika dunia ya mtoto na kazi zao huonesha tajiriba za watoto kwa mfano majukumu yao katika jamii, maadili na shughuli zao nyumbani na shuleni. Huwa na dhana au wazo kuu linalohusu na kuwavutia watoto. Kwa mfano hadithi *ya Kijana Mpelelezi* (Wamitila 2007*)* inaonesha upelelezi uliofanywa na Kangwana kuhusu nyumba ya shangazi yake. *Usiku wa manane (*Kobia 2010*)* nayo ni

matukio katika safari ya usiku waliofunga msimulizi, mnuna wake na mama yao kwenda jijini Biro kwa mwaliko wa halati.

Mandhari ya hadithi za watoto aghalabu huhusishwa na shughuli au matendo ya kawaida ya watoto na maisha yao ili watoto halisi wanaposoma hadithi hizo waweze kujitambulisha nazo. Maeneo haya ni kama vile shuleni, nyumbani, porini, uwanjani, safarini na njiani. Kwa mfano, katika hadithi zote mbili tulizochunguza matukio yake yanafanyika katika mazingira ya kawaida ya watoto.

Hadithi za watoto huogozwa na fantasia. Sifa hii inamaanisha kuwahadithi hizi huwa na mambo mengi ya kiajabuajabu ambayo hayatokei katika maisha ya kawaida ya kila siku. Wamitila (2003) anasema kuwa ni matukio yanayovuka mipaka ya uhalisia na tajiriba ya watoto na ambayo ni msingi mkubwa katika fasihi inayokiuka ulimwengu wa kawaida na kuweka wasomaji wake katika ulimwengu wa kimazingaombwe na ndoto. Sifa za kustaajabisha ni jambo la kawaida katika fasihi ya watoto. Fantasia hufanya hadithi hizi ziwafurahishe watoto kwa kuwa huwahamisha kutoka ulimwengu wa kawaida na kuweka katika ulimwengu wa usimulizi. Katika hadithi ya *Kijana Mpelelezi* (Wamitila 2007), Kangwana aliota ndoto ya kutisha, upepo mkali ulivuma na kuyumbisha bembea alimokuwa ametulia. Shangazi yake alimwendea kwa mundu tayari kumkata halafu bembea ikakatika na kujipata mikononi mwa mzee Majungu.

Mvuto unaotokana na hadithi za watoto ni sifa muhimu sana katika fasihi za watoto na hujenga ilhamu ya kupenda kusoma hadithi hadi mwisho. Wamitila (2002) anaeleza mvuto kuwa ni hisia azipatazo msomaji kuhusiana na mhusika fulani. Kwa kawaida ikiwa msomaji amempenda mhusika fulani atakuwa na hamu ya kutaka kufuata ili kujua yatakayompata mhusika huyo. Dhana ya mvuto katika hadithi huhusisha vipengele vingi. Kazi hiyo lazima iwe na mtazamo wa watoto. Watoto huwa fikra tofauti na watu wazima na huenda wasifurahishwe na mambo yanayowapendeza watu wazima. Wao basi huvutiwa na kazi iliyoandikwa na mwandishi anayejali matamanio yao kulingana na wakati wanamoishi. Mvuto mkubwa katika fasihi ya watoto hutokana na uwezo wa mwandishi na

nguvu zake katika usimulizi wa kazi yake. Usimulizi huu hushughulikia mambo ambayo ni muhimu tu katika kujenga hadithi.

Watoto hufurahishwa na hadithi zilizo na matendo ya ujasiri ukiambatana na migogoro inayotokea. Wamitila (2008) anasema kuwa mhimili mkubwa katika fasihi ya watoto ni tendo kuu, jasira na usimulizi wa ujasiri huo pamoja na mapambano yanayojitokeza. Wamitila (2008) anaeleza kuwa jasira ni tukio fulani la uvumbuzi na ambalo linahusishwa na safari inayokumbwa na misukosuko. Usimulizi wa hadithi unajengwa kwenye maelezo ya vile mhusika mkuu anavyokumbana na vizuizi njiani na hatimaye kuweza kushinda kwa mfano katika safari ya kutoka katika msitu fulani, matatizo ya uwindaji msituni, maisha ya uyatima bila wazazi au changamoto wanazopata shuleni. Katika *Usiku wa Manane (Kobia 2010)*, Kwa mfano safari ilijaa changamoto chungu nzima. Licha ya karaha waliyopata kwenye msitu wa Mendeki, msimulizi, mamake na mnuna wake walifika nyumbani kwa halati. Mabinamu na mabintiamu waliwakaribisha kwa bashasha tele. Katika *Kijana Mpelelezi (*Wamitila 2007), Kangwana alipata changamoto kuhusu nyumba ya shangazi iliyodhaniwa kuwa na majini. Alipambana na upelelezi na hatimaye aliweza kupata na kung'amua kiini cha uvumi huo. Mwanzo na mwisho wa hadithi hizi kwa kawaida huibua hisia za kuburudisha.

Funzo kuu la hadithi hujitokeza kwa pale mwanzoni au mwishoni mwa hadithi inayosomwa huku likimwelekeza mtoto msomaji na kumfunza maadili katika maisha yake. Watoto huvutiwa na hadithi zinazochimuza hisia na kutosheleza matarajio yao katika jamii wanamoishi. Kisa katika hadithi za watoto aghalabu husimuliwa na kuwa na kipindi kifupi kiwakati. Kwa mfano Usiku *wa Manane* (Kobia 2010*)* ni safari iliyofungwa usiku mmoja tu kuelekea jijini Biro. *Kijana Mpelelezi (*Wamitila 2007*)* ni hadithi inayojikita katika muda wa likizo ambao Kangwana na mnuna wake Maria walienda kumtembelea shangazi.

## 2.3 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Fasihi ya watoto ya Kiswahili, imewahi kuhakikiwa kupitia kazi za aina nyingi zikiwemo tasnifu za uzamili na uzamifu katika vyuo vikuu na makala katika majarida ya lugha na vitabu. Bila shaka suala la maudhui limeweza kujitokeza katika tafiti za aina tofauti. Suala

hili limewahi kujadiliwa kiusomi kwa njia nyingi tofauti lakini kila wakati linachukua mikondo tofautitofauti kulingana na malengo ya mtafiti. Kutokana na uelewa huu, mapitio ya maandishi yaliyoteuliwa katika utafiti huu yalilenga kubainisha uhalisia wa kimaudhui ili kuwekea msingi uchunguzi huu kwa kutalii jinsi kazi hizo zilivyouchangia. Mapitio haya yalipangwa kulingana na madhumuni ya utafiti ambayo ni kuchunguza uhalisia wa maudhui ya usalama katika hadithi teule za watoto za Kobia na Wamitila.

Miongoni mwa watafiti ambao maandishi na tafiti zao zilikuwa na umuhimu katika utafiti huu kwa njia moja au nyingine kuhusiana na maudhui ni Sutherland (1985), Hunt (2002), Karin (2004), Bainbridge (2005), Reynolds (2007), Bhroin na Patricia (2012), Mpesha (1996), Karuga (2005) Ngugi (2009 na 2016) Muriungi (2014), Nyaga (2017) na wengine.

Baadhi ya tafiti zao zimejihusisha na mabadiliko katika nathari za watoto nchini Kenya. Watafiti waliotajwa hapo juu walibainisha jinsi maudhui katika hadithi za watoto yamekuwa yakikua na kuakisi mabadiliko katika jamii ya Kenya. Mmoja kati ya watafiti hao ni Muriungi (2014). Katika uhakiki wake, masuala mbalimbali yanayohusu jamii yalibainika kwa kuwasilishwa kupitia kwa hadithi na kulenga maudhui yanayokusudiwa kuwafahamisha watoto kuhusu mabadiliko yaliyotokea nchini Kenya tangu nchi ilipopata uhuru. Utafiti wake ulikuwa tofauti na huu wa sasa kwa kuwa alichunguza kukua kwa maudhui kwa kuzingawa hadithi katika vipindi vitatu vya kiwakati. Vipindi hivyo ni 1966 – 1986, 1987 – 2000 na 2001 – 2008. Kusoma utafiti wa Muriungi kulichochea utafiti huu kuchunguza hadithi za watoto zilizoandikwa katika kipindi kilichofuatia utafiti wake. Hadithi teule za utafiti huu zilichapishwa mwaka 2007 – 2010.

Utafiti wa Ngugi (2016) ulichunguza usawiri wa masuala ibuka katika fasihi ya watoto. Mtafiti huyu wa fasihi ya watoto anaeleza kuwa, fasihi ni zao la wakati. Jinsi jamii inavyobadilika ndivyo fasihi inavyofaa kubadilika ili iweze kuyamulika masuala mapya yanayoibuka katika jamii. Kwa misingi hii, masuala ibuka yameanza kuwashughulisha waandishi wa fasihi ya watoto. Kutoka mwaka wa 2003, waandishi walianza kutunga hadithi zilizoshughulikia maudhui yanayolenga masuala ibuka yaliyotajwa katika silabasi ya shule za msingi iliyokuwa imefanyiwa mabadiliko mwaka 2002. Masuala ibuka

yanahusu maudhui yanayorejelea mambo ambayo yametokea katika jamii na kuiathiri. Masuala hayo ni kama vile afya na ukimwi, mazingira, haki za watoto, ajira za watoto, jinsia, dawa za kulevya, teknolojia na mikasa kama vile mioto na mafuriko (Ministry of Education, 2002). Ngugi alitumia mifano kutoka Kenya na kujadili masuala ibuka yaliyobainika kutokana na hadithi nane teule. Baadhi ya masuala hayo ni haki za watoto katika *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), Ukimwi katika *Yalianza Kimchezomchezo* (Mdari, 2001) na *Alipata Tuzo* (Ngugi, 2006), ulemavu katika *Si Kupenda Kwake* (Ngugi, 2001) na utunzaji wa mazingira katika *Ujeuri wa Mbwa* (Ngugi, 2005)

Mifano mingine inayoweza kutolewa ya hadithi zinazoakisi masuala ibuka na ambayo yanaambatana na fasihi ya watoto ni pamoja na *Siku ya Ukimwi* (Kobia, 2008), *Kusema Ukweli* (Kobia 2008) na *Usilie, Yakobo* (Mogambi, 2014) ambazo zinahusu suala la ukimwi. *Mwepesi wa Kusahau* (Matundura, 2005) na *Likizo ya Mkosi* (Matundura, 2014) ni hadithi zinazogusia suala la usawa wa kijinsia. Mifano mingine ni *Nikicheka, Anacheka* (Ngugi, 2003), *Usicheze na Moto*! (Ngugi, 2003). Utafiti wa Ngugi ulikuwa tofauti na huu kwa kuwa ulitalii jinsi masuala ibuka ya kiusalama yanavyosawiriwa katika hadithi ilhali huu utachunguza iwapo masuala ibuka ya kiusalama yanayojumuishwa katika hadithi za watoto yana uhalisia. Hata hivyo, matokeo ya utafiti huo yalikuwa muhimu kwa kuwa yalibainisha kupanuka kwa maudhui kutegemea mabadiliko ya kiwakati na maisha ya jamii. Utafiti huo uliupa msukumo utafiti huu wa sasa kuchunguza iwapo kupanuka kwa maudhui kuliweza kuibua uhalisia katika hadithi za watoto zilizoteuliwa.

Utafiti wa Nyaga (2017) ulihusu maudhui ya masuala ya kisiasa katika vitabu vilivyoteuliwa vya fasihi ya watoto. Malengo ya utafiti huo yalikuwa kufafanua jinsi maudhui katika vitabu teule vya fasihi ya watoto yanavyoendeleza itikadi za kisiasa; kutathmini jinsi waandishi wa kazi teule za fasihi ya watoto wanavyotumia lugha kuendeleza itikadi za kisiasa na kueleza namna wahusika katika vitabu teule vya fasihi ya watoto wanavyoendeleza itikadi za kisiasa. Utafiti huo uliweza kuthibitisha kuwa itikadi za kisiasa huweza kujitokeza katika hadithi za watoto za Kiswahili kupitia maudhui, mbinu za lugha zilizotumiwa katika hadithi na jinsi wahusika walivyosawiriwa katika hadithi hizo. Utafiti wa Nyaga uliufaa huu wa sasa kwa kuwa ulibainisha kuwa itikadi za kisiasa

huwepo katika hadithi za watoto. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wa Nyaga kwa kuwa ulionyesha kuwa, ni kweli kuna maudhui ya kisiasa katika hadithi za watoto,na uhalisia wake basi upo katika jamii halisi. Utafiti wa Nyaga ulijishughulisha tu na kuwepo kwa maudhui ya kisiasa lakini huu ulijishughulisha na kuwepo kwa maudhui mengine ya kiusalama kama vile maudhui ya vitisho, vita na usalama wa kitaifa.

Mwangi, J.W (2013) akitafitia riwaya za Said Ahmed Mohammed *Babu alipofufuka* alijadili uhalisiajabu katika wahusika na mandhari katika riwaya hizi teule. Mtindo wa uhalisiajabu unatumika kuyashughulikia mambo ambayo hayangeweza kuwekwa wazi kwa mtindo wa kiuhalisia. Utafiti huu ni tofauti na wa sasa kwa kuwa matukio yake yamepiga hatua nyingine na vile vile unahusiana na huu kwa kuwa uhalisiajabu ni kiwango kinachofuata uhalisia hakiki na uhalisia wa kijamaa.

Herman,(2018), katika makala yake alitumia lugha na mbinu nyingine za kisanaa kufikisha ujumbe kwa jamii hasa ya watoto. Wakati mwingine alivuka mipaka ya uhalisia kwa kuhusisha wahusika na mambo ya kinjozinjozi au kifantasia kwa maksudi. Mtindo huu wa kutumia fantasia katika kazi za fasihi ni kinyume kabisa na wanataaluma wanaoamini katika ukweli na uhalisia. Na wafuasi wa nadharia ya uhalisia wanadai kuwa mwandishi au msanii wa kazi za fasihi anapaswa kutoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku. Mwandishi huyu anashughulikia dhima na lengo la mbinu ya fantasia kifasihi. Utafiti huu ni tofauti na wa sasa unaoongozwa na nadharia ya uhalisia.

Haji, (2018) alifanya utafiti kwa nia ya kuchunguza uhalisia wa utabaka katika tamthilia mbili J*anga la Werevu* (2011*)* na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000*)*. Malengo mahsusi yalikuwa ni kuchambua uhalisia wa utabaka. Utafiti wa sasa unachunguza uhalisia wa maudhui ya usalama katika kazi ya Kobia na nyingine ya Wamitila. Utafiti wake ulihusiana na huu wa sasa kwa kuwa tafiti zote zilitumia nadharia ya uhalisia wa kijamaa na matokeo yake yalibainisha hali halisi katika jamii. Migogoro ya kiuchumi, kisiasa, kiitikadi na utabaka, umaskini, ufisadi, ukiukwaji wa haki katika jamii na utafutwaji wa haki kwa nguvu za umma.

Karoki (2014) alitafiti kuhusu uhamaji na uhamiaji katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* iliyoandikwa na Adam Shafi.Utafiti huu ulichangia sana huu wa sasa kwa kuwa umeongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa ambayo hujikita katika utoaji wa picha halisi ya maisha ya binadamu. Utafiti huu umeshughulikia matatizo yanayowakumba wanajamii kutokana na uhamaji na uhamiaji. Utafiti huu unatumia nadharia ya uhalisia kuweka wazi uhalisia wa maudhui ya usalama.

Utafiti wa Mpesha (1996) ulihusika na fasihi ya watoto kama ilivyotokea nchini Tanzania.Mpesha aliweka wazi ukuaji na kuendelea kwa fasihi ya watoto nchini Tanzania kwa kuchunguza vitabu vya hadithi za watoto vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Mpesha alitambua majukumu ya fasihi ya watoto yanayopatikana katika jamii. Utafiti wa Mpesha uliufaa huu kwa kuwa ulikubali kuwa vitabu vya hadithi za watoto huonesha hali halisi ya jamii na vile vile kuwa hadithi zile si ngano tu za kupitisha wakati bali ni kioo cha mambo yanayoendelea katika jamii. Hata hivyo utafiti wa Mpesha ni tofauti kwa kuwa ulionesha ukuaji na maendeleo ya fasihi ya watoto ilhali huu unahusu maudhui ya kiusalama na kisiasa katika fasihi ya watoto.  Ili kuleta uelewa kwa watoto kuwa jamii itapata maendeleo endelevu iwapo amani itadumishwa miongoni mwa wanajamii. Kazi hizi ziliufaa utafiti huu kwa kuwa zilichunguza na kutoa mielekeo muhimu kuhusu maudhui katika utunzi wa fasihi ya watoto.

Osman, Yan na Kassim, (2017) wametafiti kuhusu kazi za watoto wa Malaysia na kupata kuwa kazi za watoto huko zilianza mapema kidogo zikilinganishwa na za Uingereza. Utafiti huu una uhusiano mkubwa na wao kwa kuwa unasaidia kulenga lini kazi za fasihi ya watoto za Kiswahili zilivyoandikwa.

Kazi ya Sutherland (1985), ilihusu itikadi za kisiasa katika fasihi ya watoto na ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa ilionyesha kuwa maudhui ya kisiasa ni miongoni mwa yale yanayozua shida za kiusalama katika nchi nyingi ulimwenguni.

Hunt (2002) anaeleza kuwa hadithi za watoto ni muhimu kwa vile zina uwezo wa kuwashawishi watoto wanaozisoma kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja.

Anadai kuwa hadithi zinazokiuka maadili yanayopaswa kuadilisha watoto zinapaswa kudhibitiwa kwa kuondolewa sokoni au kupigwa marufuku kwa vitabu kama hivyo. Kazi hii ya Hunt iliufaa utafiti huu kwa njia mbili kuu. Kwanza, iliupa msukumo utafiti huu kwa kufafanua kuhusu umuhimu wa fasihi ya watoto. Utafiti huu uliangazia fasihi ya watoto kutokana na umuhimu wake katika kuangazia masuala ibuka yanayomzunguka mtoto katika jamii anamokulia. Pili, iliuelekeza utafiti huu katika kutambua maudhui ambayo yalikuwa hayakubaliki katika hadithi za watoto na ambayo yalifaa tu katika hadithi za watu wazima.

Karin (2004) akielezea kuhusu fasihi hii ya watoto anasema lazima vitabu vya fasihi hii vijikite katika maudhui ya kimaadili. Kimsingi, lazima ile fasihi iongee na watoto. Kitabu kilichoandikiwa watoto hulenga kuwasiliana na watoto na kufikisha ujumbe kwao. Aidha Karin, (2004) alifafanua kuhusu maana ya maudhui ya fasihi ya watoto. Ufafanuzi wake uliufaa utafiti huu katika kuuwekea vigezo vya kuchunguzia maudhui katika hadithi zilizoteuliwa.

Kwa jumla, mapitio haya ya maandishi kuhusu maudhui katika fasihi ya watoto yaliuwezesha utafiti huu kubainisha suala la uhalisia wa maudhui. Hii ni kwa sababu yalitoa sifa za kimaudhui zilizotarajiwa katika hadithi za watoto. Sifa zilizobainishwa katika mapitio haya ziliuelekeza utafiti huu kutambulisha maudhui yalivyo katika jamii. Maudhui ya kisiasa, kiupelelezi na kiusalama yalionyesha kuwa fasihi ya watoto si fantasia tu lakini ina msingi katika matukio halisi na katika jamii ya mwandishi. Fasihi ya watoto ni fasihi maalumu inayolenga hadhira ya watoto na huwa na jukumu la kuwaadilisha, kuwaburudisha na kuwafunza. Kidesturi fasihi ya watoto imekuwa ikishughulikia maudhui yanayohusu ujenzi wa maadili kati ya watoto lakini katika karne ya ishirini fasihi hii yaelekea kubadilika na kuchukua mpangilio tofauti wa kimaudhui. Maudhui ya kisiasa, na yanayohusu upelelezi yamejipenyeza.

### 2.4 Msingi wa nadharia

Nadharia zilizoongoza utafiti huu zilitolewa maelezo katika sehemu hii. Buliba, Mayaka na Riro (2014) wanaeleza kuwa nadharia ni njia ya kutazama kitu katika taaluma yoyote.

Katika utafiti nadharia ni kama dira ambayo inatumiwa kumpa mtafiti mwelekeo wa kufikiria suala maalumu katika utafutaji wa maarifa. Mtafiti huamua nadharia itakayomfaa kutazamia na kuitathminia kazi ya fasihi anayotafitia kutokana na madhumuni yake. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na ile ya Sosholojia ya fasihi

### 2.4.1 Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa

Nadharia ya uhalisia wa kijamaa ilitokana na mawazo ya Karl Marx. Mwanafalsafa aliyemtangulia Karl Marx na kuiathiri falsafa yake kwa kiasi kikubwa alikuwa G.F Hegel. Hegel aliamini kuwa vitu vyote vinavyopatikana humu ulimwenguni huwa na picha hafifu ya vitu hivyo kama vinavyodhihirika katika dunia ya kinjozi na kuwa vitu hivyo huendelea kukua na kubadilika kuuelekea ukamilifu. Kuna uwiano kati ya fikra ya Hegel kuhusu ukamilifu wa kitu na ile ya Darwin kuhusu maendeleo ya mwanadamu. Baada ya uchunguzi wake kuhusu wanyama Darwin alihitimisha kwamba binadamu amefikia kiwango alichoko cha ukamilifu kwa kuvipitia viwango vya awali vingine visivyokuwa vikamilifu.

Wanafalsafa wengine walioshungulikia uhalisia wa kijamaa ni Fuerbach na Maxim Gorki. Fuerbach alieleza kuwa vitu vyote vinatokana na kuishia mumu humu duniani. Maxim Gorki anasema chochote tunachopata chenye uzuri wa kutamanika kimeumbwa au kuendelezwa na mtu. Ni jambo la kuhuzunisha kwamba mtu amezalisha na kuendeleza dhuluma dhidi ya mtu. Maxim Gorki, anasema kwamba chochote kizuri kinachotamanika humu ulimwenguni kimeumbwa kuelezwa na binadamu tu. Uhalisia wa kijamaa huonesha uhalisia wake kwa uelekeo wa kijamaa. Uhalisia wa kijamaa huonesha mambo katika misingi ya kijamaa kwa namna ya kupinga matabaka hivyo njia ya uzalishaji mali humilikiwa kwa usawa.

Huwa na muundo fulani wa kihistoria ambao huonekana kama mgogoro kati ya matabaka. Ili jamii iweze kubadilika na kuwa na maendeleo lazima iwe na historia fulani kutoka katika hatua moja kwenda nyingine. Mfano, Karl Max na Fredrick Hegel walisema jamii zote ulimwenguni ilibidi zipitie katika hatua ili jamii iweze kufikia usawa na hivyo kuleta maendeleo katika jamii. Wanasisitiza kuwa maisha ni matendo na ubunifu wake

unaonesha ukuaji wa binadamu na kuweza kuibuka mshindi katika mapambano na nguvu za kweli. Lengo la nadharia hii ni kuonesha namna waandishi wanavyowatumia wahusika mbalimbali katika jamii wanavyotakiwa kuwa watu wenye ujuzi na mbinu mbalimbali za kuweza kupambana na matatizo yanayowakumba katika jamii kwa mfano maswala ya unyonyaji, rushwa, matabaka na umaskini ili mwisho wake waweze kuyashinda matatizo hayo. Chanzo kikuu cha mivutano ni uzalishaji mali. Hii hutokea pale ambapo tabaka la chini linapojaribu kupambana na tabaka la juu ili kuweza kumiliki nyenzo mbalimbali za uzalishaji mali kama vile mashamba na viwanda, hali ambayo hupelekea tabaka la chini kupata usawa katika jamii.

Fasihi husawiriwa kama silaha ya kupinga masuala yasiyofaa ya dhuluma, unyonyaji na uonevu. Waandishi wengi wa fasihi huandika kazi zao kwa nia ya kulikomboa tabaka la chini kutoka kwa mikono ya dhuluma, unyonyaji na uonevu ili kuweza kuendeleza usawa katika tabaka hilo tawaliwa katika nyanja zote za maisha, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Hutazamia maisha ya baadaye na ujezi wa jamii mpya yenye raha na ufanisi. Uhalisia wa kijamaa huelekeza jamii yake kuacha mambo yanayozuia maendeleo katika jamii husika kwa kuwaonesha wahusika wanaopigana kuleta mabadiliko katika nyanja zote za kimaisha yaani kifikra, kiuchumi, kisiasa na kiutamanduni ili wawe na jamii moja yenye raha na ufanisi.

Mihimili ifuatayo ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa ndiyo inayoongoza tungo za kifasihi. Moja ni wahusika wa kimaendeleo wanaonuia kupindua na kubadilisha hali yao ya maisha. Pamoja na kusawiri matukio kihistoria, wahusika hutekeleza matendo yao kitabaka. Uhalisia wa kijamaa hushughulikia masuala ya makabwela ambao ni mafukara wa ulimwengu wenye mtazamo wa kuendeleza udikteta wao. Nadharia hii huonesha binadamu kwa kiuyakinifu ambapo wahusika hutumiwa kama vipaza-sauti vya waandishi na hupuliziwa uhai jamii, kwa mfano wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaouelewa. Nadharia hii huonesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu, hii inamaanisha kwamba mtu ataweza kuwa mshindi au ni mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote anayofanyiwa. Lugha inayotumiwa katika uhalisia wa kijamaa huendeleza malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jamii husika.

Yanayoshulikiwa katika hadithi yanafaa yamhusu na yalandane na tajiriba ya mtoto ili aweze kufaidika kutokana na hadithi anapoisoma. Watoto hupendezwa na wahusika mashujaa. Wao huvutiwa na hadithi zilizo na mhusika anayeshinda hali ngumu inayomkabili. Hadithi kama hizo huwapa moyo na kuwaonesha kuwa hata na wao wanaweza kufaulu hata changamoto zinapowakabili. Waandishi wa hadithi za watoto hujiweka katika ulimwengu wa watoto na kazi zao huonesha tajiriba za watoto kama vile kazi zao katika jamii, maadili na shughuli zao shuleni na nyumbani. Hata hivyo hali hii inaendelea kubadilika na fasihi ya watoto inachukua mielekeo mipya kimaudhui na kifani katika karne ya ishirini na moja. Wametokea waandishi wa fasihi ya watoto wanaoandika kuhusu masuala halisi ya kisiasa na yale ya kiupelelezi katika fasihi ya watoto. Waandishi hao ni kama vile Kobia, J. (2010) ambaye amehusisha maudhui ya siasa katika kazi za watoto lakini kwa njia isiyo wazi katika hadithi ya *Usiku wa Manane* na Wamitila K W. (2007) anayekumbana na maswala ya upelelezi katika Kijana *Mpelelezi.*

### 2.4.2 Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi

Nadharia ya pili ambayo imeongoza utafiti huu ni Sosholojia ya fasihi. Swingerwood (1975), alisema kuwa mwasisi wa nadharia ya Sosholojia ya fasihi ni Taine. Taine alilinganisha fasihi na kioo na akasema kuwa fasihi huonesha yanayoendelea katika jamii. Alitaka kuweka wazi kuwa fasihi huakisi maisha ya jamii kama vile kioo kinavyoonesha sura ya mtu anayejitazama. Taine vilevile aliyachukua, akayaunda upya na kuyaendeleza mawazo ya Germaine de Stael. Kwa mujibu wa *Encyclopaedia Britannica Online* (2011) de Stael alionesha majukumu ya nadharia ya Sosholojia ya fasihi katika kazi yake ya *The Influence of Literature Upon Society* (1835). Alisema kuwa kazi za kifasihi zilizo nzuri zapaswa kuonesha uhalisia wa kimaadili, kihistoria, hali ya utamaduni, uchumi na hata siasa katika jamii ambamo kazi yenyewe imezalika na kupatikana.

Mtaalamu aliyehusika kwa mapana na nadharia hii ya Sosholojia ya fasihi na kusemwa na wasomi wengi kuwa ndiye mwaasisi wa nadharia hii ni Georg Lukacs katika karne ya ishirini. Lukacs aliathiriwa na maelezo ya Karl Marx kuhusu maendeleo ya kijamii na migogoro inayotokana na utabaka. Kazi nyingi za uhakiki za Ki-marx ni za kijamii na zinaonesha maisha ya jamii jinsi yalivyoonekana nyakati zile.

Coser (1963) anasema kuwa nadharia hii hutumiwa kuweka wazi jinsi uandishi wa fasihi unavyohusiana na mambo ya kijamii kama vile imani, mila, desturi, maadili, elimu na mikondo yote ya kijamii. Anasema kuwa fikra na ubunifu wa mwandishi huongozwa na uzoefu wake wa mambo katika jamii anayoandika habari zake. Warren na Wellek (1973) wanasema kuwa uhusiano kati ya fasihi na jamii unapatikana katika kauli kama aliyotoa De Bonald kuwa fasihi ni kielelezo cha yanayopatikana katika jamii. Kwa hivyo ni muhimu kuisawiri fasihi kama linalozalika kutokana na jamii na ambalo huwa limeathiriwa na mazingira ya jamii hiyohiyo. Mtunzi vilevile kwa kuwa ni mmoja wa wanajamii huandika kuhusu hali ilivyo katika maisha yake na katika wakati wake.

Hivyo, fasihi huwa na utangamano mwingi na masuala ya kijamii na hivyo maudhui katika fasihi huwa yanaambatana na masuala ya kijamii. Hii inamaanisha kuwa mwandishi hupata maudhui ya kazi yake kutokana na mambo yanayoendelea katika jamii yake. Nadharia ya Sosholojia ya fasihi ilinifaa katika kushughulikia kazi hii hasa kulingana na mihimili yake mikuu ambayo huongoza matukio yanayoonesha maisha halisi ya jamii na pili wahusika wanaotenda vitendo vinavyowakilisha matendo ya kweli na ya kila siku ya watu katika jamii. Kazi za fasihi nilizochunguza, kwa mfano zinaweka wazi uhalisia wa maudhui na kuonesha jinsi yanavyopatikana katika jamii halisi.

## SURA YA TATU

## 3.0 MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti zilizojadiliwa kwenye sura hii ya tatu, zilitoa ufafanuzi wa jinsi shughuli za utafiti huu zilivyopangiliwa na kutekelezwa. Gay, Mills na Airasian (2006) na Buliba, Mayaka na Riro (2014) wanaeleza kuwa utafiti wa kitaaluma huzingatia mbinu na mikakati maalumu kuibua elimu mpya na maarifa mageni. Mbinu za utafiti basi ni taratibu zinazotakiwa kuzingatiwa katika mchakato mzima wa utafiti. Kwa hivyo, sura hii imelenga kubainisha njia zilizotumika kuweka pamoja data muhimu ya uchunguzi na kuichanganua mintarafu ya malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na misingi ya nadharia. Sura hii pia imejadili muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kikundi lengwa na namna sampuli ilivyoteuliwa, data ilivyokusanywa na jinsi uchanganuzi wa data ulivyofanywa.

### 3.2 Muundo wa Utafiti

Kimsingi, utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Gay, Mills na Airasian (2006) wanafafanua kuwa utafiti wa aina hii hutoa maelezo au ufafanuzi wa mambo yanavyopasa kuwa na aghalabu hutumiwa tafiti za lugha na fasihi zinavyofanywa. Baada ya kusoma vitabu vya hadithi vilivyoteuliwa, udondozi wa maudhui katika kila hadithi ulifanywa ili kuchunguza na kuchambua maudhui ya kiusalama na maswala mengine yanayohusiana nao katika hadithi za watoto. Tathmini ya maudhui ilifanywa kupitia kwa mtazamo wa nadharia ya Uhalisia wa Kijamii. Hatimaye maelezo yalitolewa kuhusu maudhui hayo kufuatana na maswali ya utafiti na kisha baadaye, matokeo na mapendekezo yaliwasilishwa.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Kimsingi, utafiti huu umekuwa wa maktabani. Mtafiti alikusanya na kusoma kwa mapana vitabu tofautitofauti vya hadithi za watoto vilivyokusudiwa kusomwa na wanafunzi wa shule za msingi gredi ya nne hadi ya sita. Pamoja na vitabu vya hadithi, alisoma vitabu na matini mbalimbali vilivyohusiana na mada ya utafiti na nadharia za utafiti ili kupata uelewa mpana na wa kina kuhusu mada iliyotafitiwa. Matini hizi zilikuwa msingi uliomwezesha mtafiti kuimarisha na kupanua maarifa na uelewa wake kuhusu maswala ya fasihi ya

watoto yakiwemo yale yanayohusu maudhui ya kisiasa, kiusalama na kiupelelezi ya fasihi ya watoto. Matini hizi zilipatikana baada ya mtafiti kutafuta kwenye maktaba, maduka ya kuuzia vitabu na kwenye mtandao wa tovuti.

Baadhi ya marejeleo yalitokana na kununua vitabu na majarida yaliyokuwa na makala kuhusu fasihi ya watoto. Mtafiti pia aliazima baadhi ya marejeleo kutoka kwa wasimamizi wake na kujenga hazina ya marejeleo katika mahali pake pa utafiti.

### 3.4 Kikundi Lengwa

Kulingana na Kothari na Gaurav (2014), kundi la utafiti lililolengwa ni mkusanyiko mzima unaohusishwa katika utafiti. Watafitiwa ni kundi la watu au vitu vinavyochunguzwa ili kupata taarifa muhimu katika utafiti. Hivyo basi, data ya utafiti hutoka kwa kundi la utafiti. Katika utafiti huu, kikundi lengwa cha utafiti kilikuwa vitabu vingi tofauti vilivyo na hadithi zilizoandikiwa watoto nchini Kenya ambavyo vinapaswa kusomwa na watoto wa umri wa miaka tisa hadi kumi na mmoja (shule ya msingi gredi ya nne hadi darasa la nane) na ambavyo vina maudhui yanayotafitiwa.

### 3.5 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ulitegemea aina ya data iliyohitajika na mtafiti katika utafiti wake na upatikanaji wa data hiyo. Data iliyokusanywa kwa ajili ya uchunguzi huu ilitumia sampuli lengwa au makusudi. Sampuli lengwa ni vielelezo ambavyo viliteuliwa kwa kudhamiria. Mtafiti alikuwa na imani kuwa vilitoa data iliyomwezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake. Sampuli lengwa ilipatikana kwa kuteua na kusoma vitabu vingi vya hadithi vinavyokusudiwa kusomwa na watoto wa madarasa ya juu yaani ya sita, saba na nane katika shule za msingi ambavyo viliandikwa kuanzia mwaka wa 2006 nchini Kenya. Vitabu vilivyoteuliwa kupitia sampuli lengwa ni *Usiku wa Manane* (Kobia 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila 2007). Viliteuliwa kwa kuwa vinahusu siasa, vitisho, vita na matukio yanayohatarisha usalama wa kitaifa. Upekee wa vitabu hivi kimaudhui ni kuwa vinahusu maudhui ya kisiasa yanayolandana na vita vya kikabila baada ya uchaguzi mkuui wa mwaka 2007 nchini Kenya. Baadhi ya vitabu vilishughulikia maudhui hayo kwa kutumia wahusika wanyama ilhali *Usiku wa Manane (Kobia 2010)* kimetumia wahusika binadamu.

Kitabu cha *Kijana Mpelelezi* (Wamitila 2007), kiliteuliwa kwa kuwa mwandishi amempa mtoto nafasi ya kuwalinda watu wazima na kutokea kuwa shujaa wa upelelezi.

### 3.6 Ukusanyaji wa Data

Walliman (2001) anafafanua umuhimu wa kukusanya data kwa makini kwa vile habari zilizokusanywa ni marejeleo muhimu katika kutoa ithibati kwenye utafiti ili kupata data itakayotegemewa. Vitabu vilivyoteuliwa vilisomwa kwa kina ili kupata ufahamu wa ndani wa maudhui katika hadithi hizo. Maudhui au matukio yanayohusu siasa, vitisho, vita, yanayopelekea ukosefu wa usalama wa kitaifa na upelelezi yalikusanywa. Maswala ya kuleta suluhu na amani yalichunguzwa. Data iliyokusanywa ndiyo iliyotumika katika kujibu maswali ya utafiti. Utafiti huu ulihusisha kwa kiasi kikubwa data za msingi.

### 3.7 Uchanganuzi wa Data

Kila hadithi ilielezwa kwa muhtasari baada ya kusomwa na kisha kufuatiwa na shughuli ya kudondoa data kutoka kila kitabu kwa kuzingatia mpangilio wa madhumuni na maswali ya utafiti. Data ya utafiti huu ilichanganuliwa kwa misingi ya uchanganuzi wa matini au wa nyaraka.

### 3.8 Maadili ya utafiti

Kila taaluma huwa na mwongozo na mwenendo wake unaotarajiwa na wataalamu husika. Walliman (2001) anaeleza kuwa utafiti huzingatia maadili hasa ya uwajibikaji na uaminifu. Utafiti huu umekuwa wa maktabani hivyo, mtafiti alihitajika kuwa na vibali vilivyomruhusu kuingia katika baadhi ya maktaba. Alijisajili pia kama mtumiaji wa maktaba wa muda katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kulipa ada inayohitajika. Vibali hivyo ni pamoja na kibali cha chuo kikuu cha SEKU. Kama mwanafunzi wa Chuo cha SEKU, atahitajika kuonesha kadi ya uanafunzi ili kuruhusiwa kuingia.

### 3.9 Hitimisho

Katika sura hii, ufafanuzi wa jinsi utafiti ulivyotekelezwa umetolewa na kuweka wazi mbinu za utafiti zilizotumika kukusanya, kuchambua na kuchanganua data za utafiti huu.

Kwa ufupi, sura hii ilifafanua kuhusu muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kikundi lengwa, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data.

# SURA YA NNE

## 4.0 UCHANGANUZI WA DATA NA MATOKEO

### 4.1 Utangulizi

Sehemu hii inashughulikia ubainishaji wa data na matokeo ya utafiti ambapo madhumuni ya kwanza ambayo ni kubainisha masuala ya usalama yaliyothihirishwa na waandishi wa riwaya zilizoteuliwa yameoneshwa. Utafiti huu ulishughulikia pia madhumuni ya pili ambayo ni kuchunguza na kubainisha uhalisia wa maudhui ya usalama katika jamii katika kipindi husika. Wamitila (2016) anafafanua maudhui kama jumla ya masuala yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi. Katika utafiti huu maudhui ni yale mambo au masuala yanayozungumziwa katika hadithi zilizoteuliwa na ambayo yanahusishwa na usalama wa wananchi katika jamii. Kwa Mfano katika *Usiku wa Manane* (Kobia 2010) maudhui yanahusu upigaji kura, migogoro ya uchaguzi, vitisho, vita na usalama wa kitaifa. Katika *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007) maudhui yanayohusiana na upelelezi, vitisho, propaganda na chuki katika jamii zinadhihirishwa. Sehemu hii pia inashughulikia madhumuni ya tatu ambayo ni kuelezea jinsi watoto wanaohusishwa na maudhui ya usalama wanavyosawiriwa kupitia hadithi zilizoteuliwa za watoto za Kobia, J. na Wamitila K.W.

#### 4.1.1 Maudhui ya Siasa

Wamitila, (2016) anafafanua siasa kama mfumo na namna ya kuendesha shughuli za nchi kwa wanaoongoza. Utafiti huu unatoa kauli kuwa siasa inahusu itikadi inayofuatwa na viongozi wa nchi. Uchanganuzi wa maudhui katika hadithi ya *Usiku wa Manane (Kobia 2010)* unatokana na siasa hasa za uchaguzi mkuu. Maudhui ya kisiasa basi yalizuka kutokana na ghasia baada ya uchaguzi zilizoleta ukosefu wa usalama katika hadithi hiyo. Kwa muhtasari, katika hadithi ya *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010), msimulizi wa hadithi, mamake na mnuna wake walifanya safari kwenda kumtembelea halati wakati wa likizo ya Agosti. Safari yao ilitokana na mwaliko wa halati kupitia kwa arafa ya simu. Katika safari hii iliyofanywa usiku tunakutana na matatizo yanayowakumba watu baada ya uhasama wa kisiasa baina ya jamii mbili. Uhasama huo ulichochewa na wanasiasa wawili waliotaka kuwa seneta.

Mwandishi ametalii maudhui yanayotokana na siasa hasa za uchaguzi mkuu. Khaisie (2018) anaeleza kuwa, uchanguzi mkuu husababisha mihemko na taharuki miongoni mwa wananchi. Wakati mwingine mihemko hii husababisha ghasia. Khaisie (2018) anatoa mfano kuwa mwaka wa 2007 ghasia zilizuka nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu na kutikisa umoja na mshikamano wa kitaifa kutokana na matamshi ya chuki yaliyoleta mgawanyiko miongoni mwa jamii. Hadithi ya *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010) ambayo iliandikwa baada ya mwaka wa 2007, ilibainisha maudhui ya kisiasa yanayoakisi ghasia zilizozuka baada ya uchaguzi mkuu. Msimulizi wa kisa ni mwandishi mwenyewe. Akiwa njiani alipata fursa ya kujionea eneo lililokuwa na vyumba vingi vya mahema. Sehemu hii tunachunguza Uhalisia wa maudhui ya vita vya kikabila katika hadithi hii ya *Usiku wa Manane (Kobia, 2010).*

Katika safari hii tunakutana na matatizo yanayowakumba watu baada ya uhasama wa kisiasa baina ya jamii mbili. Uhasama huo unachochewa na wanasiasa wawili waliotaka kuwa maseneta. Msimulizi wa kisa ni mwandishi mwenyewe. Akiwa njiani, alipata fursa ya kujionea eneo lililokuwa na vyumba vingi vya mahema. Alishangaa ni kwa nini palikuwa na watu wengi waliokuwa wanaishi katika mahema jinsi hiyo. Mama yake alimweleza kuwa pahali penyewe paliitwa Mahema na ilikuwa kambi ya wakimbizi. Walioishi pale walikuwa ni wakimbizi wa ndani ya nchi waliohama makwao kwa ajili ya kutafuta usalama baada ya uhasama baina ya jamii ya Wahoi na Waheri. Msimulizi alielezewa kuwa wanasiasa wawili waliogombea useneta katika kaunti ya Karandinga, kila mmoja akitaka kiti hicho ndio waliochochea jamii ya Wahoi na Waheri kugombana. Mzozo ulianza wakati Tandabelua ambaye alitoka katika jamii ya Wahoi alipodai kuwa yeye ndiye aliyeshinda uchaguzi wa seneta na wakati huo huo Hifadhi naye akawaeleza wafuasi kutoka jamii yake kuwa ndiye aliyeshinda kiti hicho cha uongozi na wala si Tandabelua. Hapo ndipo vurugu ilipozuka.

Maudhui haya yalibainika kwa kuchunguza hadithi hii kwa mtazamo wa mhimili wa kwanza na pili wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa kwamba fasihi ni kioo cha jamii. Katika utafiti huu mwandishi amepenyeza maswala ya siasa za uchaguzi mkuu katika hadithi za watoto. Kulingana na IEBC (2012), njia ya uchaguzi inayotumiwa nchini Kenya ni upigaji

kura kwa njia ya demokrasia. Mpigaji kura humchagua kiongozi ampendaye kwa kuweka alama kwenye nafasi kando ya picha yake katika orodha ya wagombea uchaguzi wa cheo hicho katika karatasi maalumu ya kupigia kura Viongozi waliochaguliwa huchukua mamlaka mbalimbali kuambatana na vyeo walivyopewa ili kuongoza jamii kwa kufanya maamuzi kuhusu maendeleo ya nchi. Maamuzi ya kisiasa yanayofanywa huelekeza sera za nchi na hivyo ustawi wa nchi hutegemea maongozi ya kisiasa yaliyomo. Kwa vile wafuasi wa mgombeaji kiti ambaye hakufanikiwa kuchaguliwa huhisi kama wataachwa nje ya serikali, uchaguzi wa viongozi wa kisiasa katika mataifa mengi huibua mihemko mikali miongoni mwa jamii ambapo makundi tofauti hupingana kuhusu nani achaguliwe. Kutokana na mirengo tofauti ya kisiasa, mgawanyiko hutokea katika jamii. Migawanyiko hii mara nyingi huchochewa na viongozi wenyewe wanaotafuta kura, kama inavyoakisika kutokana na maudhui katika *Usiku wa Manane (2010)*

Watoto huathiriwa sana, zaidi ya watu wazima wanaposhuhudia mizozo au vita aidha nyumbani au katika jamii. Athari za kimawazo na kihisia huwakumba na huwafanya kubadilika kitabia kulingana na umri wao. Waiyaki na Onyango (2017) wanataja kuwa watoto walioshuhudia vita baada ya uchaguzi mkuu wa 2007/2008 kupitia kwa runinga na mitandao ya kijamii na vilevile wale waliokumbana nayo wenyewe huenda mzongo wa mawazo ukazidi kuwarudiarudia katika maisha yao yote.

Japo watoto hawapigi kura, wao hujipata katikati mwa ghasia za baada ya uchaguzi kama vile waliochomwa katika kanisa la Kiambaa mjini Eldoret Kenya mnamo 2008 kwa mujibu wa runinga ya Citizen. Masuala yanayozungumziwa yana uhusiano mkubwa na uchaguzi mkuu katika mataifa mengi hasa ya kiafrika.  Uchaguzi mkuu hufanyika katika nchi nyingi ulimwenguni kwa taratibu mbalimbali kulingana na katiba za nchi hizo. Kwa mfano, kulingana na katiba ya Kenya (2010) (Republic of Kenya, 2010) uchaguzi mkuu huwa kila baada ya miaka mitano. Viongozi huchaguliwa kushikilia nyadhifa sita ambazo ni wadhifa wa Urais, ule wa Ugavana, Useneta, ubunge, Uwakilishi wa wadi naule wa uwakilishi wa wanawake mbungeni.  Kifungu cha 38 cha Katiba ya Kenya kinashauri kuwa kila mwananchi aliyefikia umri wa kuwa na kitambulisho ana haki na jukumu la kuwachagua

viongozi awapendao. Maudhui ya Unafiki wa wagombea vyeo pia yamejipenyeza sana katika riwaya hizi teule na ni mojawapo wa masuala yanayokosesha usalama katika nchi.

Wamitila (2016) anafafanua unafiki kama hali ya kujifanya mkweli kumbe sivyo. Katika hadithi ya *Usiku wa Manane (2010)* ukurasa wa 12 hadi 21, unafiki unaotokana na tabia ya wanasiasa unadhihirika tunapokutana na abiria wanaozumgumza ndani ya basi kuhusu viongozi wao waliosababisha mapigano baina ya wananchi na kueneza chuki. Abiria mmoja aliwaeleza wenzake kuwa viongozi hao wawili, Hifadhi na Tandabelua bado ni marafiki na kuwa wao wawili wameshakubaliana kuwa Hifadhi ahifadhi kiti cha useneta naye Tandabelua awe naibu wake. Isitoshe tayari wao walikuwa matajiri kinyume na wakimbizi wale waliokuwa wakiishi kimaskini katika mahema kwenye kambi ya wakimbizi. Wale walitengemea wahisani wawasaidie na kuwakimu kwa kuwapa chakula, mavazi na dawa.

Unafiki unadhihirika kutokana na viongozi hawa wawili kwa sababu hawakumbuki hata kidogo wananchi waliowachagua ambao walikuwa wanakabiliana na matatizo mengi katika kambi ya wakimbizi. Wao waliishi katika majumba ya kifahari wakati wakimbizi wakiishi katika vibanda bila kuonyeshwa upendo tena na viongozi wao. Watoto huwa na usalama katika jamii ambapo mizozo na vita havipo katika familia na vilevile katika jamii. Iwapo watalelewa katika jamii yenye fujo basi huenda wakaiga na kuwa wenye mizozo baadaye.

Kulingana na Bhroin na Patricia (2012) maudhui ambayo hayajengi maadili yafaayo miongoni mwa watoto hayafai na kutokana na ukweli huu unafiki si tabia njema. Watoto wanapopata habari hiyo kuhusu vigogo wa kisiasa wa kiwango cha kitaifa wakiwa wanafiki na wabinafsi na kwamba wanapiganisha watu kwa faida yao wenyewe watakuwa wakielewa kuwa wanafaa kujiepusha na mambo yanayoleta mafarakano kutokana na uchochezi wa wanasiasa. Hawatakubali kutumiwa kuzua fujo na vigogo hao.

Mzozo kuhusu mshindi ni nani ni jambo lililotokea katika jamii ya Karandinga baada ya uchaguzi mkuu**.** Kwa mtazamo wa mhimili wa pili wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa,

maudhui haya katika *Usiku wa Manane (2010)*, yanahusu matukio ya baada ya uchaguzi mkuu wa kisiasa, kulikuwepo na uchaguzi wa useneta ambapo wawania wakuu walikuwa Tandabelua na Hifadhi. Baada ya uchaguzi huo, mzozo unazuka wakati walioshindwa wanakataa matokeo. Katika ukurasa wa 12, Tandabelua ambaye alitoka jamii ya Wahoi alidai kuwa yeye ndiye aliyeshinda uchaguzi wa useneta na wakati huo huo, Hifadhi naye akawaeleza wafuasi kutoka jamii yake kuwa alihifadhi kiti hicho cha uongozi baada ya kumshinda mpinzani wake. Katika uhalisia wa mambo, kisa hiki ni usawiri wa mizozo inayotokea baada ya uchaguzi mkuu katika baadhi ya mataifa hasa ya Kiafrika.

Kutokana na utafiti huu, mfano huu unaweza kulinganishwa na tukio la baada ya uchaguzi wa Urais nchini Kenya mwaka 2007. Mzozo huu wa 2007 hadi 2008 kuhusu ni nani aliyeshinda ulizuka na kuathiri sana usalama wa nchi ya Kenya.Hii ni baada ya Rais Mwai Kibaki kutangazwa mshindi katika uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 27 Disemba 2007.Wafuasi wa mpinzani mkuu wa Kibaki katika uchaguzi huo mheshimiwa Raila Odinga wa chama cha Orange Democratic Movement (ODM) alipinga matokeo hayo. Jambo hili lilishuhudiwa na wajumbe wa kimataifa, Raila Odinga alisema kuwa kura ziliibiwa na kwamba ndiye aliyekuwa mshindi. Mwenyekiti wa tume ya uchaguzi ECK iliyosimamia uchaguzi wakati huo pia alikubali kuwa hakujua aliyeshinda uchaguzi huo ingawa alikuwa amemtangaza Kibaki kuchukua hatamu za uongozi jioni ya tarehe 30 Disemba 2007.

Upande wa upinzani walitangaza maandamano kupitia kwa mitandao ya kijamii. Mizozo basi ilionekana wazi katika miji mikuu ya Kenya, Mombasa, Eldoret, Kericho, Kisumu, Nakuru na sehemu kadhaa jijini Nairobi. Vita baina ya waluo na wakalenjin waliokuwa wafuasi wa mheshimiwa Raila na wagikuyu waliomuunga mkono rais Kibaki wa chama cha PNU vilipamba moto. Polisi nao waliingilia kati na katika harakati za kutawanya walio na fujo basi vifo vingi vilitokea. Watu zaidi ya elfu moja, mia sita walifurushwa kutoka makwao na kulazimika kuishi katika mahema kama wakimbizi wa ndani ya nchi (Nation 27/1/2008). Mwaka uliofuatia Aprili 2008 viongozi hawa wakiongozwa na mjumbe wa kimataifa Koffi Annan waliweka mkataba ulioitwa National Accord and Reconcilliation Act (2008) (makubaliano ya kitaifa na mardhiano) kuwa Kibaki ahifadhi kiti cha urais na

Raila awe Waziri Mkuu katika serikali ya muungano huku wakigawana mamlaka (Cooke, J .2009).

Kutokana na utafiti huu, mfano huu pia unaweza kulinganishwa na tukio la baada ya uchaguzi wa Urais nchini Kenya mwaka wa 2013 ambapo mzozo wa ni nani aliyeshinda ulipelekwa katika mahakama ya juu. Mahakama iliamua aliyekuwa ametangazwa mshindi ahifadhi ushindi. Uchaguzi katika *Usiku wa Manane* (2010) basi ni usawiri wa hali halisi inayotokea katika baadhi ya mataifa ambapo baada ya uchaguzi kufanyika na mshindi kutangazwa, mizozo huibuka katika jamii kuhusu aliyeshinda uchaguzi.

Katika *Usiku wa Manane (2010)* usaliti unadhihirika kutokana na mazungumzo ya abiria ambayo yanaangazia suala la viongozi waliochaguliwa kuwasahau wananchi. Abiria wanafika mahali ambapo barabara ya kutoka Mahema hadi Gajo ilikuwa na mashimo makubwa na wanasikika wakiteta, kulalamika na kujibizana wenyewe kuwa barabara ile ni mbovu ilhali wanalipa kodi. Wanadai kuwa pesa zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara zinapotea. Hii ilikuwa na maana kuwa wale waliopewa pesa za mradi huo ili wawahudumie raia waliwasaliti kwa kukosa kutekeleza mradi waliotakiwa kutekeleza kwa ajili ya kuwaondolea wananchi shida. Wanadai kuwa miezi sita ilikuwa imepita tangu mwanakandarasi kupewa zabuni ya kukarabati barabara hiyo lakini hakuwa ameanza kazi licha ya kuwa tayari alikuwa amelipwa kiasi cha mamilioni ya pesa. Wanatoa maoni kuwa ule si ufisadi tu bali ni usaliti kwa raia.

Usaliti kwa raia unaoneshwa pia katika *Usiku wa Manane (Kobia, 2010*) kupitia kwa wagombea wa useneta Tandabelua na Hifadhi.Waliwaacha wakimbizi wa ndani ya nchi kuselelea katika mahema walikoishi kwa dhiki bila kuwapa msaada wa kudumu. Wananchi walipigana kwa ajili yao lakini walipochukua hatamu za uongozi wakawasahau. Hivyo, maudhui haya ni usawiri wa hali halisi inayotokea katika baadhi ya mataifa ambapo baada ya uchaguzi kufanyika na mshindi kutangazwa, mihemko huibuka katika jamii kuhusu mshindi ni nani. Baada ya upigaji kura, vitisho kama vile vinavyojulikana kama ghasia za baada ya uchaguzi, hutokea. Mzozo huzuka kuhusu aliyeshinda kiti cha urais huku upande uliosemekana kushindwa ukikataa kukubaliana na matokeo na kusema kuwa

umenyang'anywa ushindi. Maudhui hayo kutokea katika fasihi ya watoto ni vizuri ili waelewe kwani wao hujipata wakiathirika mizozo kama hiyo itokeapo katika jamii wanamoishi.

Kwa mujibu wa Khaisie (2018), kulikuwa na tatizo sugu nchini Kenya ambapo machafuko baada ya uchaguzi kama vile uchaguzi wa mwaka 2007 yalishuhudiwa. Hili hutokana na viongozi walioshindwa na wenzao katika uchaguzi kukosa kukubali kushindwa na badala yake kuzusha ghasia kati ya wanajamii. Nchini Kenya wanajamii walizozana na idadi kubwa kufurushwa makwao na kujipata katika mahema. Baada ya kupatanishwa rais Kibaki na waziri mkuu Raila Odinga waliwasaliti raia waliokuwa katika mahema. Hakuna mpango kamilifu wa kuwarudisha wakimbizi makwao uliofanyika na woga kuhusiana na uchaguzi mkuu huwepo kila baada ya miaka mitano.

Maudhui zaidi kama haya kuhusu viongozi waliochaguliwa kuendelea kujinufaisha wenyewe huku wakiwasaliti wananchi yanaendelea kujitokeza katika kisa kuhusu msitu wa Lailuba katika *Usiku wa Manane (Kobia, 2010)*.

Msitu huu ulikuwa umeharibiwa na watu waliokata miti ya kiasili na kuchoma makaa kinyume na sheria. Miti hasa iliyokuwa imekatwa kwa wingi ni ile iliyokuwa ndani ya msitu na makaa yenyewe yalichomwa kwa njia ya siri maana yalichomewa ndani msituni. Watu walioharibu msitu hawakushitakiwa. Inaelekea waliokata miti walishirikiana na viongozi wenye ushawishi mkubwa. Uharibifu wa msitu ulisababisha mto Lailuba uliotoka katika msitu huo kukauka. Abiria walilalamika kuwa serikali ilikuwa imeshindwa kukomesha uharibifu wa msitu Lailuba. Serikali ilikuwa imekosa kuwajibika katika kuhifadhi mazingira. Kutowajibika katika maongozi ya kisiasa kulikuwa kumesababishwa na viongozi kujali maslahi yao wenyewe ya kujinufaisha na mali ya umma bila kujali maslali ya waliowachagua. Maudhui ya kutowajibika kwa viongozi wa kiserikali ni usaliti.

### 4.1.2 Maudhui ya vitisho

Mbali na maudhui ya kisiasa, maudhui ya vitisho yamejitokeza katika hadithi za *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007). Matukio kama vile

maandamano yanayosababisha majeruhi, mauaji, matamshi ya chuki na ugaidi ni mifano bayana. Kubainishwa kwa maudhui ya vitisho ambayo yanasababisha hofu ni njia moja ya kuwajasirisha watoto na kujipanga jinsi ya kupambana na hali ngumu zijazo katika jamii zetu halisi. Hadithi ya *Usiku wa Manane (2010)* inaakisi vitendo vya watu wazima katika jamii wanaozusha vitisho baada ya uchaguzi mkuu. Hadithi hii inaonesha jinsi wawania uchaguzi walioshindwa, ambao ni watu wazima hukataa matokeo na baadaye kuanzisha maandamano wanayodai kwamba ni ya amani lakini mara nyingi yameishia kuvuruga amani na kusababisha uchochezi unaopelekea uharibifu wa mali, watu kupoteza mali yao, kujeruhiwa na wengine kuuawa.

Maudhui na uchochezi yanadhihirishwa na Tandabelua aliyekuwa mhoi na Hifadhi aliyetoka katika jamii ya waheri. Matamshi hayo yalisababisha chuki za kikabila na vurugu. Mzozo ulizuka wakati Tandabelua alipowachochea wahoi kwa kuwambia kuwa yeye ndiye aliyeshinda uchaguzi wa Seneta na wakati huo huo Hifadhi naye akawachochea wafuasi kutoka jamii ya waheri kwa kudai kuwa alishinda kiti hicho. Vita vilizuka baina ya waheri na wahoi baada ya matamshi ya Hifadhi na Tandabelua (ukurasa wa 12). Vita vya kikabila vinatokea Kenya kutokana na chuki na uchochezi kutoka kwa wanasiasa. Bayne, S. (2008), alieleza kuwa uchochezi ulisababisha vita katika maeneo ya Bonde la Ufa baina ya wakalenjin na Agikuyu, vikosi vya kigaidi vilijitokeza kutetea jamii zao katika miji kama vile Nakuru na Naivasha. Matumizi ya nguvu kutawanya wapiganaji na vikosi vya usalama viliacha wengi wakiwa wafu na wengine viwete.

Ugaidi na utekaji nyara ni mojawapo ya masuala yanayosababisha kiwewe katika jamii. (Reynolds, 2017). Visa vya ugaidi vimezungumziwa katika *Usiku wa Manane (2010)* ambapo usalama wa wasafiri kwenye basi ulihatarishwa wakati wateka nyara walivamia abiria usiku wa manane na kuteka nyara basi lao. Basi liliingizwa msituni katika sehemu ya Mendeki ambapo abiria waliporwa mali yao yote waliyokuwa wamebeba. Kwa bahati nzuri, magaidi hao hatimaye walishambuliwa na polisi huku mmoja wao akiuliwa. Wengine walijeruhiwa na baadhi yao walikamatwa. Kutokea kwa maudhui yanayohusu ugaidi ni uhalisia katika jamii hapa nchini kenya Taifa Leo 13 Septemba 2021 yaonesha viongozi wa kiislamu wakiishutumu serikali kwa kuongezeka kwa visa vya kupotea kwa

washukiwa wa ugaidi. Kwa mujibu wa matangazo haya ugaidi na utekaji nyara katika hadithi za watoto zilizoteuliwa ni uhalisia mtupu. Visa vya ugaidi vinavyowasilishwa vina uwezo wa kuweka watoto wanaolengwa kusoma hadithi husika tayari kupambana navyo katika maisha.

### 4.1.3 Maudhui ya vita

Katika hadithi ya *Usiku wa Manane (Kobia, 2010)*, kuna vita vikali baina ya wanajamii. Mwingiliano wa kimaudhui unaonyesha uzito wa suala hili la vita vya kikabila katika mtazamo wa mwandishi. Katika hadithi ya *usiku wa manane (2010)*, tunaelezewa kuwa:

> "Ninakumbuka vita vilizuka baina ya Waheri na Wahoi baada ya matamshi ya Hifadhi na Tandabelua Mheri alikuwa akimtafuta Mhoi kwa kisu kama mwindaji anavyomtafuta swara. Mhoi alipomwona Mheri damu ilisimama. Alimfukuza kwa mawe ungedhani ni mtu anayewinga ndege waharibifu wasile mawele yake" (Ukurasa 12)

Katika hadithi hii, wanasiasa walisingizia kuwa walikuwa wakipigania demokrasia. Kwa hakika, kule kulikuwa kutumia neno demokrasia vibaya. Ile kama walivyosema baadhi ya wananchi katika ukurasa wa 14, haikuwa demokrasia bali ilikuwa ni kutumia neno demokrasia kama kejeli. Mwishowe, wananchi wasiokuwa na hatia waliumia. Watu walitoroka makwao wakaishi katika mahema katika hali ya kusikitiwa wakiwa wakimbizi uhasama baina ya jamii ya Wahoi na Waheri ulipozidi kama inavyosimuliwa katika ukurasa wa 17. Nchini Kenya, wakati wa vita vya kikabila baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007, watu wa jamii moja walishambuliwa, kuuawa na nyumba zao kuchomwa katika ghasia hizo. Uhalisia wa kijamii unaonesha kuwa kati ya mambo yanayosababisha migogoro ya kisiasa katika jamii ni chuki za kikabila (Muriungi, 2014). Maoni ya utafiti huu ni kuwa kutokana na madaraka makubwa yanayokuwa katika urais, kila jamii inahisi kuwa inapaswa kupata nafasi ya mmoja wao kuwa rais ikidhani itafaidi. Jamii mbalimbali huwa zimeishi kwa amani, umoja na upendo lakini matokeo ya uchaguzi wa urais yanapotangazwa yanazusha vurugu kwa muda baina ya jamii hizo. Vurugu hii husababisha

kufukuzwa kwa baadhi ya watu kutoka maeneo fulani na kuwepo kwa wakimbizi wa kisiasa wa ndani kwa ndani katika taifa.

Watu wengi huishi katika jitimai kubwa baada ya mali yao kuharibiwa, kufurushwa makwao na nyumba zao kuchomwa kutokana na vita vya kikabila. Maudhui haya yana uhalisia. Ilibainika kuwa kuna watoto wanaoishi katika hali za kusikitikiwa hasa wale wanaoishi kwenye mahema kutokana na vita vya kikabila.Kwa mujibu wa runinga ya Citizen 28/1/2008 watoto waliteseka pamoja na watu wazima walipojipata katika mahema katika uwanja wa Afraha mjini Nakuru baada ya kufurushwa makwao.(Tazama Kiambatisho A chenye anwani; A child's exposure to violence can lead to lasting physical,mental and emotional harm.'Daily Nation' 27 December 2007) Ni vyema watoto kupata kusoma jinsi wenzao walivyoteseka ili kutafuta suluhu ya matatizo yanayowakabili maishani.

Maudhui kuhusu vita vya kikabila yametawala kwa mapana na marefu hasa katika mahema. Alishangaa ni kwa nini palikuwa na watu wengi waliokuwa wanaishi katika mahema jinsi hiyo. Mama yake msimulizi alimweleza kuwa pahali penyewe paliitwa Mahema na ilikuwa kambi ya wakimbizi. Walioishi pale walikuwa ni wakimbizi wa ndani ya nchi waliohama makwao kwa ajili ya kutafuta usalama.ICJ februari 18,2020 wanaeleza kuwa ghasia zilizotokea baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007-2008 katika nchi ya Kenya zilisababisha maafa mengi, wanawake na watoto wa kike kunajisiwa na kubakwa, mali kuporwa na wakenya kuwa wakimbizi katika nchi yao. Katika hali hiyo ya vita, ilikuwa vigumu sana kuripoti visa hivyo kwa polisi au hata kupata matibabu ya dharura. Kuna wahusika wachache sana ambao walishtakiwa mahakamani lakini kesi zikatupiliwa mbali kwa sababu ya ukosefu wa ushahidi wa kutosha.

Katika hadithi ya *Usiku wa Manane,* mzozo ulizuka wakati Tandabelua alipowaambia wahoi kuwa yeye ndiye aliyeshinda uchaguzi wa seneta na wakati huo huo Hifadhi naye akawachochea wafuasi kutoka katika jamii ya waheri kwa kudai kuwa alishinda kiti hicho. Vita vilizuka baina ya waheri na wahoi ili kulipiza kisasi kwa ajili ya uchaguzi na kura kuibiwa. Uhalisia wa kimaudhui unajitokeza katika hadithi hii k wani jamii imekubwa na

fujo na ghasia kutokana na kulipiza kisasi kisiasa mwaka baada ya mwaka.Kulingana na utafiti uliofanywa na Halmashauri ya Umoja Duniani na kuripotiwa kwenye idhaa ya Deutchewelle News (2017)vita vimekuwa vikizuka baada ya miaka ya uchaguzi mkuu nchini Kenya.Vita vilizuka mwaka wa 1992,1997,2008,2013 na 2017.Mwaka 2017 watoto Samantha Pendo na Stephanie Moraa (Tazama kiambatisho B chenye anwani; Watoto Kuangamia Katika Vurugu Baada ya Uchaguzi Mkuu,'Deutche welle News' 2017) waliangamia kutokana na matumizi ya nguvu nyingi za polisi wakikabilina na magenge ya kikabila katika vita baada ya uchaguzi mkuu. Katiba mpya ya Kenya (2010) ilitoa mamlaka ya uongozi na ya kifedha kwa gatuzi 47 ili kupunguza uhasama unaotokana na mamlaka yote kuselelea katika kiwango cha kitaifa.

### 4.1.4 Maudhui kuhusu usalama wa kitaifa

Usalama wa kitaifa ni mojawapo wa masuala ibuka hasa kutokana na ripoti za mara kwa mara zinazopeperushwa na vyombo vya Habari. Vyombo hivyo vikiwemo redio, runinga na magazeti, huwa na habari za hapa na pale kuhusu visa vya uhalifu, ugaidi, itikadi za kidini na za kijamii, utekaji nyara, ajali za barabarani na uharibifu wa mazingira.

Utafiti huu unaonyesha kuwa, hali hiyo ya ukosefu wa usalama katika jamii na hasa katika kiwango cha kitaifa imeanza kuchochea maudhui katika hadithi za watoto. Mathalani, masuala ya usalama wa raia nchini ndio yanayoangaziwa pakubwa zaidi katika hadithi ya *Usiku wa Manane (Kobia, 2010)* pamoja na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila, 2007) Mwandishi anaonyesha vipindi vya wasiwasi, uoga na maumivu kutokana na ukosefu wa usalama unaosababishwa na viongozi wanaopinganisha wanainchi. Tunakutana na watu walio katika hali ya kusikitikiwa kutokana na madhara ya vita nchini mwao. Raia wa kawaida wanaumia na wengine kuuawa. Watoto wanaumia kutokana na ghasia za baada ya uchaguzi, ingawa hawakuwa wamepiga kura.

Katika hadithi ya *Usiku wa Manane (2010),* baada ya uchaguzi wa seneta, wawania wakuu, Tandabelua na Hifadhi, walikosa kukubaliana matokeo. Vita vya kikabila vilivyotishia usalama wa kitaifa vilizuka na ndivyo vinavyoangaziwa kwa mapana na marefu katika hadithi hii. Jamii mbili zilipigana vita vikali na kupelekea wananchi wasiokuwa na hatia

kuumia, wengine kuuawa na wengine wakafukuzwa na kuachwa bila makao wakawa wanaishi katika kambi za mahema kama wakimbizi. Raia wanasawiriwa wakieleza wasiwasi wao katika mazungumzo baina ya abiria wanaosafiri kwenye gari la umma. Katika mazungumzo hayo masuala mengi kuhusu usalama wa kitaifa yanajadiliwa hasa kuhusu kuhangaishwa kwa raia na wengine kufukuzwa makwao, kuchomewa nyumba zao na hata kuuawa.

Katika hadithi ya *Kijana Mpelelezi (2007)*, Kangwana na Maria walipofika kwa shangazi walikutana na mambo mengi kuhusu nyumba ya shangazi. Waligundua kuwa majirani walikuwa na wasiwasi kuhusiana na nyumba hiyo. Watu walisema palikuwa na majini pale na kwa sababu hiyo, nyumba hiyo iliogopwa. Jambo hili lilikuwa na tisho la kuhatarisha maisha ya Kangwana kwa kuwa hakuna aliyejua kulikuwa na siri gani katika nyumba ya shangazi.

Hadithi ya *Usiku wa Manane* (2010) kwa mfano inasimulia jinsi watu walivyopoteza mali yao kama vile mashamba, nyumba na vitega uchumi walivyokuwa navyo. Maisha yao yalihatarishwa kutokana na ukosefu wa usalama uliotokana na ghasia za baada ya uchaguzi ambao ulifanyika lakini watu wakakosa kukubaliana mshindi ni nani. Ithibati moja inapatikana katika ukurasa wa 24 ambapo katika soko la Karumaindo, abiria walipewa dakika chache wajipatie chamcha. Hapa ndipo msimulizi alikutana na kiwete mmoja aliyekuwa akiomba pesa. Kiwete huyo alisimulia kuwa hakuzaliwa akiwa na ulemavu, alikuwa mtu mwenye mali na watoto lakini baadaye akajipata akiwa hana chochote kwa kuwa mali yake yote ilichomwa wakati wa ghasia za kisiasa na hata hakujua watoto wake walipo. Kiwete huyo alikuwa mmojawapo wa waathiriwa wengi wa ghasia za kisiasa zilizozuka kati ya waheri na wahoi. Kisa kingine kinapatikana wakati basi walimokuwa wakisafiria abiria kuelekea mjini Biro lilitekwa nyara lilipofika katika sehemu ya Mendeki, majambazi waliowateka nyara walichukua pesa zote ambazo kondakta alikuwa amekusanya kutoka kwa abiria na kisha kuwatisha na kuwapora abiria wenyewe mali yao kama vile rununu, pesa taslimu, saa za mikononi, mikufu, pete na bangili.

Waathiriwa wa vita vya kikabila wanasawiriwa wakiishi katika mahema kwenye kambi ya wakimbizi kwa njia iliyohatarisha usalama wao wa afya na kwa njia isiyowapa matumaini. Kibanda kimoja kilichoishi familia moja ndicho kilichokuwa sebule, jiko, bafu na sehemu ya kulala. Magonjwa mengi yaliwapata watu walioishi katika kambi ya mahema. Waliugua maradhi ya kipindupindu na malaria. Waathiriwa walitegemea wahisani kuwapelekea chakula na misaada mingine waliyohitaji kama vile mablanketi, dawa na vyandarua. Huu ni uhalisia mtupu kwa kuwa ni mambo yanayotokea nchini yakishuhudiwa na watoto wanaonuiwa kusoma hadithi hii.

Suala la ongezeko la joto duniani ni suala linalosumbua jamii. Wasafiri katika hadithi ya *Usiku wa Manane (2010)* walifika mahali palipokuwa na joto kama tanuri na walijihisi kama mikate iliyookwa ndani ya jiko hadi wengi wao wakavua makoti. Kadhalika, safarini walipitia kwenye msitu uliojulikana kama Lailuba ambao ulikuwa umeharibiwa na wachoma makaa. Watu walikata miti ya kiasili na kuchoma makaa. Mto uliotoka katika msitu huo ulikuwa tayari umekauka kabisa. Mto kukauka ilikuwa ni hatari kwa kuwa watu na mifugo wangeathirika. Haukuwa na hata tone la maji. Watu walikuwa wamelima kwenye mianzo ya chemchemi ya maji ya mto huo. Jambo hili lilihatarisha usalama wa wanyama, miti na hata watu kwa kuwa maji ni uhai. Aidha, kutokana na mazungumzo ya abiria, serikari ilihitajika kuingilia kati na kukomesha uharibifu huo. Uhalisia unabainika katika uchanganuzi wa hadithi ya *Usiku wa Manane (2010)* kwa mtazamo wa mhimili wa nne wa nadharia ya uhalisa wa kijamaa. Matukio yanayoleta athari na hatari ya ongezeko la joto duniani yanabainika.

Suala la usalama wa mazingira ni ibuka na muhimu na linafaa kuangaziwa katika hadithi za watoto, maudhui kuhusu mambo ambayo serikali inafaa kuyafanya kuhusu uharibifu wa misitu ya umma yakieleweka na watoto itakuwa bora zaidi. Jambo ili la utunzaji wa mazingira linaambatana na malengo ya elimu shuleni ambapo kulingana na mtaala wa Kiswahili katika shule za msingi; (Ministry of Education, 2019) lengo la nane kati ya malengo manane ya kitaifa ya elimu ni kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira. Watoto watakuwa vipaza sauti vya kueneza habari hii katika jamii

Ajali nyingi barabarani husababishwa na utepetepu wa madereva. Katika hadithi ya *Usiku wa Manane (2010)*, kuna dereva mmoja ambaye aliendesha gari kwa mwendo wa kasi kupita kiasi huku akijinaki. Dereva huyo, ambaye hakujali usalama wa wasafirini, alisababisha ajali watoto wakishuhudia. Hadithi za Kobia J. na Wamitila K.W zinazungumzia maudhui ya siasa, vitisho, vita na usalama wa kitaifa huku wakionekana kupendelea maudhui yatokanayo na masuala ibuka katika jamii.

### 4.2 Usawiri wa wahusika watoto

Lynch-Brown na Carol (1999) wanaeleza kuwa wahusika ni waigizaji katika kazi ya fasihi. Naye Wamitila (2016) anaboresha fasili hii kwa kutoa kauli kuwa viumbe katika hadithi huitwa wahusika. Mwanafasihi huwabuni viumbe hawa na kuwaweka katika mandhari ambayo yatafanikisha ufikiaji wa maudhui anayokusudia. Kutokana na vitendo anavyowafanyisha wahusika, maneno anayowasemesha na jinsi anavyofanya watagusane. Bakize (2014) anaeleza kuwa ingawa hadhira ya watoto huvutiwa na hadithi zenye wahusika wanyama, wengi wao hupendelea hadithi kuhusu binadamu hasa zile zenye wahusika wa rika lao.

Ni muhimu hadithi iwe na wahusika mseto wa wavulana na wasichana na kadri iwezekanavyo isawiri usawa wa kijinsia ambapo hakuna mhusika anayesawiriwa kama duni kutokana na jinsia yake. Inapendekezwa na wataalamu kama vile Lynch-Brown na Carol (1999) kuwa wahusika wakuu ambao ni watoto wawe na umri unaolingana na wa watoto wanaolengwa katika hadithi husika. Bakize (2014) anaendelea kueleza kuwa japo fasihi ya watoto huhusisha wahusika wa aina nyingine wakiwemo wanyama, mazimwi, na hata watu wazima hapa na pale, wengi wa wahusika hasa wahusika wakuu huwa ni watoto wenyewe ili kuweza kuvutia hadhira lengwa. Wahusika watoto wanaohusishwa na maudhui ya usalama wanasawiriwa ifuatavyo katika riwaya za *Usiku wa Manane* (Kobia, 2010) na *Kijana Mpelelezi* (Wamitila2007)

#### 4.2.1 Mtoto kupewa majukumu ya kiupelelezi

Katika hadithi ya *Kijana Mpelelezi (2007)* Kangwana na Maria wanaalikwa na shangazi yao ambaye alikuwa na jumba la ajabu kumtembelea wakati wa likizo. Azma ya

Kangwana kwenda kwa shangazi yake ilikuwa kupeleleza ukweli kuhusu nyumba hiyo. Kangwana akiwa shuleni alikuwa ameigiza mchezo kama mpelelezi. Safari hii ilikuwa nafasi yake kuupeleleza ukweli kihalisia. Walipokuwa huko walikabiliana na mambo chungu nzima kuihusu nyumba hiyo. Watu katika jamii walikuwa na hofu kuhusiana na nyumba ile. Ilisemwa kuwa ilikuwa na majini na hivyo watu waliiogopa. Kangwana aliamua kuchukua ile fursa ya kumtembelea shangazi yake kuchunguza siri ya nyumba hiyo na hatimaye akafanikiwa kutambua chanzo cha sauti ambazo zilisikika usiku na ambazo hakuna mtu mwingine aliyekuwa ameweza kugundua chanzo chake hapo awali.
Kupitia kwa nadharia ya sosholojia ya fasihi, mwandishi anataja mambo yanayoonesha maisha halisi ya jamii ambapo watoto na pia watu wazima huhusishwa na mambo yasiyo na ukweli ambayo huleta fitina, chuki na pia ukosefu wa usalama. Kangwana alikuwa na tabia ya kupenda kupeleleza hata alikuwa akirejelewa na wenzake kwa lakabu ya kijana mpelelezi.

Walipofika kwa shangazi walikutana na mambo mengi kuhusu nyumba hiyo. Waligundua kuwa majirani walikuwa na wasiwasi kuhusiana na nyumba hiyo. Watu walisema palikuwa na majini pale na kwa sababu hiyo, nyumba hiyo iliogopwa. Kangwana aliamua kuchukua nafasi aliyopata ya mwaliko kupeleleza siri kamili ya nyumba ya shangazi yake. Jambo hili lilikuwa la kuhatarisha maisha yake kwa kuwa hakuna aliyejua kulikuwa na siri gani katika nyumba ya shangazi. Mhusika mtoto amehusishwa na upelelezi na hili lilifungua ukurasa mpya katika fasihi ya watoto. Hii ni kama vile mwandishi Mohammed Said Abdulla alivyofanya kuhusiana na upelelezi katika kazi zake za fasihi ya watu wazima kwa mfano *Siri ya Sifuri, (1974) Kisima cha Giningi (1968) na Mzimu wa Watu wa Kale (1982).*

### 4.2.2 Mtoto kusawiriwa kama jasiri

Vitendo vya upelelezi ambavyo Kangwana alifanya ili kuleta usalama ni kama vile kuwahoji watu wazima na vilevile kuamka usiku kuchunguza chanzo cha kelele. Kangwana ambaye ni kijana mdogo, anamhoji mfanyakazi wa nyumba ya shangazi aliyeitwa Kibibi wakati shangazi yake alipokuwa hayupo. Kumhoji shangazi akiwa hayupo kunaashiria kuwa Kangwana alikuwa na nia ya kujua siri fulani kuhusu maisha ya shangazi

yake. Kumhoji Kibibi kulimsaidia Kangwana kujua kuwa jumba lile la shangazi mbeleni lilikuwa limemilikiwa na mzungu mmoja aliyejulikana na wanakijiji kwa jina Kitili. Kangwana alifanya upelelezi ule kwa kuulizia kuhusu uvumi kuwa jumba lile lilisemwa kuwa lilikuwa na mazimwi tangu wakati wa mzungu huyo. Alielezewa kiini cha uvumi huo. Kangwana alimuuliza Kibibi mazimwi huwa na sura gani. Alitaka kujua kama ile sura aliyokuwa ameona usiku ya mtu mwenye kurunzi na mavazi meupe ina uwezekano wa kuwa sura ya zimwi. Kibibi alijibu kuwa hajawahi kuyaona mazimwi hayo ingawa anasikia yanakaa kama binadamu na huweza kuvaa na kutembea kama watu na hata yanaweza kubeba kurunzi usiku. Baada ya kumhoji Kibibi, Kangwana aliamua kuwa angekaa huko mpaka agundue siri ya nyumba ya shangazi. Alitaka kujua chanzo cha zile sauti za ajabu na chanzo cha wasiwasi wa watu kuhusu ya nyumba ya shangazi kati ya mambo mengine.

Kangwana pia alimhoji mfugaji kwa jina Kasa kwa kumuuliza iwapo alikuwa amesikia habari zozote kuhusu nyumba ya shangazi yake. Kasa alisema ni kweli alikuwa amesikia ina majini. Kangwana alimuuliza Kasa habari za mzee Majungu na akajibiwa kuwa yule alikuwa mzee mbaya. Ni wakati huo ambapo Kangwana aligundua kuwa yule mzee hakumpenda shangazi yake na kuwa alikuwa mwenye wivu dhidi yake. Habari hii ilikuwa muhimu kwa Kangwana na hivyo aliamua kupepeleleza kiini cha wivu huo na kugundua kuwa babake mzee Majungu alikuwa mfanyakazi wa Kitili na kwamba ndoto ya Majungu ilikuwa kuachiwa shamba hilo na mzungu. Habari hizi zilikuja kumfaa Kangwana baadaye katika upelelezi wake.

Kangwana hatimaye alimdadisi yule mzee Majungu mwenyewe ambaye alikuwa amekutana naye hapo awali na ambaye alikuwa na habari kuhusu nyumba ya shangazi na pia alionyesha kuwa na wasiwasi mwingi. Mzee Majungu ambaye jina lake kamili lilikuwa Kenga wa Majungu alimwambia jambo ambalo Kangwana aliamini lingemsaidia kujua siri ya nyumba ile. Alimwambia kuwa zamani nyumba ile ilikuwa ya mzungu ambaye alikuwa na majini na akaendelea kudai kuwa mazimwi hayo yalibaki pale hata mzungu alipoondoka. Mazimwi hayo yalijitokeza usiku yakiwa yameshika kurunzi na yalisikika yakilia kama paka. Hapo Kangwana akamaizi lazima nyumba ya shangazi ilikuwa na

majini. Yeye mwenyewe Kangwana alikuwa ameona mtu aliyekuwa ameshika kurunzi usiku na pia alikuwa amesikia sauti kama ya paka.

Baada ya hapo haikuchukua muda mrefu Kangwana kugundua siri ya nyumba ya shangazi. Matukio hayo yote yanamsawiri Kangwana kama mwenye akili iliyozidi kawaida ya mtoto hasa anapoweza kupata fununu kuhusu siri ya nyumba ya shangazi yake jambo ambalo lilikuwa limewashinda watu wazima. Aliweza kupata suluhu ya matatizo yaliyowashinda wanajamii. Mathalani, Kangwana aliamua kuwa akiamka usiku kupeleleza chanzo cha sauti za ajabu kila akizisikia. Kangwana aliamka kutoka kwenye kitanda na kuangalia nje kupitia dirishani ndipo akagundua kuwa chanzo cha ule mwangaza ni mtu aliyekuwa nje na kurunzi gizani akitembea. Baada ya muda, mtu huyo akaenda zake. Kangwana akarudi kitandani kulala na akaota ndoto iliyomtisha. Usiku mwingine akiwa amelala, Kangwana alisikia sauti paani kama kawaida. Akaamka na kuchungulia dirishani, akaona kiumbe aliyefanana na binadamu na aliyekuwa amevalia mavazi meupe akipanda mtini. Kangwana akadhani ni yale mazimwi aliyoelezwa na mzee majungu. Baada ya muda akasikia mlio kama wa paka. Hapo akaamua kwenda kumwambia shangazi mambo aliyoyaona nje.

Wakiwa pamoja na shangazi walitoka nje kuelekea alikokuwa mtu aliyekuwa mtini akijaribu kuteremka huku wakimmulika kwa mwangaza mkali wa kurunzi. Hawakumtambua mara moja kwa kuwa alikuwa amejifunika kichwani kwa kofia kubwa nyeupe. Mtu yule alikuwa akiteremka haraka haraka na kwa bahati mbaya aliteguka akaanguka chini kwa nguvu. Walipompata na kumfungua kichwani hawakuamini macho yao. Walishangaa kuona kuwa alikuwa ni yule mzee Majungu hasa. Punde si punde, mbwa alimshambulia mzee Majungu na kumjeruhi vibaya. Kangwana aliondoka kwa shangazi yake siku ya nne baadaye kwa furaha ya kukamilisha upelelezi wake. Sauti za ajabu usiku hazikusikika tena. Mzee majungu hakuja tena. Kangwana alikuwa na hamu ya kufika shuleni amsimulie mwalimu wake kisa cha mzee majungu ili kumwonyesha kuwa alikuwa mpelelezi hodari.

Kulingana na Ngugi (2014) akimrejea Cass (1967), uadilifu katika hadithi za Watoto huhimizwa ili ionekane ya kwamba wema unakwezwa na kushinda uovu; uovu wa mzee Majungu wa kutatiza usalama wa wanakijiji kwa kuwekelea nyumba ya shangazi kuwa na mazimwi ulishindwa kupitia upelelezi wa kijana Kangwana.

### 4.2.3 Usawiri wa jinsia katika maudhui ya usalama

Jinsia ni hali ya kimaumbile ya kuwa kike au kiume Wamitila, K.W (2016), Opunde, Wandera-Simwa na Nabea (2018) wanafafanua kuwa dhana ya jinsia hurejelea uhusiano baina ya majukumu ya kuwa mume au mke huku wakifafanua kuwa dhana hii imechipuka kutokana na dhana ya uana ambayo inachunguza masuala ya kike na kiume kwa misingi ya kibayolojia na kuonesha jinsi yanavyotegemeana. Lynch-Brown na Carol (1999) wanaeleza kuwa hadithi ya watoto inafaa ihusishe wahusika wa jinsia zote mbili kike na kiume.Mitazamo ya kijinsia katika jamii imebadilika sana kiasi kwamba usawa wa kijinsia unatambuliwa kikatiba katika nchi nyingi.Mfano ni katiba ya Kenya,2010 (Republic of Kenya,2010).Kuhusisha jinsia zote ni jambo la busara na linalozuia kuendelezwa kwa ubabedume katika enzi hii kwa kuwa ni kinyume na malengo ya kitaifa ya elimu ambapo lengo la tano linaeleza kuwa elimu inafaa iimarishe usawa wa kijamii na uwajibikaji (Ministry of Education,2019). Kadhalika ni njia mojawapo ya kuimarisha malengo ya maendeleo endelevu ambapo lengo nambari 5 linahimiza kuwepo na usawa wa kijinsia na kupewa uwezo kwa wanawake na wasichana wote (United Nations, 2015).

Hii inahitajika ili kutimiza mahitaji ya watoto wa jinsia zote wanaosoma kitabu na kuwasaidia kuelewa kikamilifu zaidi mitazamo na hisia za watoto wenzao walio katika hadithi. Aidha, Taasisi ya ukuzaji mitaala ya Kenya (KICD) ambayo ndiyo huidhinisha vitabu vya hadithi vinavyofaa kusomwa shuleni, inapendekeza kuwa watoto wa jinsia ya kike wahusishwe na wasawiriwe sawa na watoto wa kiume katika vitabu. Sifa hii imehusishwa kwa kuwa wahusika watoto wa kike wanahusishwa katika hadithi teule, Usiku *wa Manane (2010)* na *Kijana Mpelelezi (2007)* sawia na wahusika watoto wa kiume.

Katika hadithi ya *Usiku ya Manane (2010)* msimulizi ambaye ni mtoto wa kike anahusika katika safari ya kwenda jijini Biro kumsalimia halati yake Koroboi. Ni katika safari hiyo

anapokumbana na maswala mbalimbali ya usalama. Msimulizi ni miongoni mwa wasafiri ambao walikumbana na suala la ongezeko la joto. Walifika mahali palipokuwa na joto kama tanuri na walijihisi kama mikate iliyookwa ndani ya jiko hadi wengi wao wanavua makoti. Kadhalika, safarini walipita kwenye msitu uliojulikana kama Lailuba ambao ulikuwa umeharibiwa na wachoma makaa. Watu walikata miti ya kiasili na kuchoma makaa. Mto uliotoka katika msitu huo ulikuwa tayari umekauka kabisa. Suala la mazingira ni suala ibuka na muhimu ambalo linafaa kuangaziwa katika hadithi za Watoto. Maudhui kuhusu mambo ambayo serikali inafaa kufanye na kuhusu uharibifu wa misitu ya umma ni maudhui yanayofaa katika fasihi ya watoto. Hii itawafanya watoto kutunza misitu na kuwakosoa wanaoharibu miti. Jambo hili ni muhimu kwa kuwa inaambatana na malengo ya elimu shuleni ambapo kulingana na mtaala wa Kiswahili katika shule za msingi (Ministry of Education, 2019), lengo la nane kati ya malengo manane ya kitaifa ya elimu ni kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira.

Katika hadithi ya *Kijana Mpelelezi* (2007) mhusika mkuu mtoto ni mvulana. Kangwana anayejitwisha upelelezi ili kuleta usalama katika nyumba ya shangazi. Yeye Kangwana na dadake Maria walipokuwa huko walikabiliana na mambo chungu nzima kuihusu nyumba hiyo. Watu katika jamii walikuwa na hofu kuhusiana na nyumba ile. Ilisemwa kuwa ilikuwa na majini na hivyo watu waliiogopa. Kangwana aliamua kuchukua ile fursa ya kumtembelea shangazi yake kuchunguza siri ya nyumba hiyo na hatimaye akafanikiwa kutambua chanzo cha sauti ambazo zilisikika usiku na ambazo hakuna mtu mwingine aliyekuwa ameweza kugundua chanzo chake hapo awali. Ujasiri alio nao Kangwana wa kupeleleza matukio katika nyumba ya shangazi ni njia mojawapo ya kuwaadilisha watoto ili waweze kupambana na mambo katika jamii bila woga.

# SURA YA TANO

## 5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sehemu hii inashughulikia muhtasari kuhusu matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza maudhui ya usalama katika fasihi ya watoto, kudhihirisha uhalisia wa maudhui ya usalama katika jamii katika kipindi husika. na mwisho kuonesha jinsi wahusika watoto wanaohusishwa na maudhui ya usalama wanavyosawiriwa.

### 5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulidhibitisha kuwa hadithi zilizoteuliwa za Kobia J.na Wamitila K. W. zina uhalisia wa kimaudhui na zimechukua mielekeo mipya.Mwandishi Kobia J. ameibuka kuwa na upekee wa kutumia hadithi za watoto kufahamisha jamii kuhusu migogoro ya kisiasa iliyoikumba nchi,sawa na fasihi ya watu wazima inavyofanya.Maudhui ya upigaji kura,udanganyifu katika uchaguzi mkuu na mzozo kuhusu mshindi ni nani yameoneshwa.Mbali na hayo,ilibainika kuwa,hadithi hizi zilisheheni maudhui ya vitisho kutokana na matamshi ya chuki, maandamano na vita vya kikabila vilivyosababishwa na mzozo uliozuka walioshindwa walipokataa kukubali matokeo.Vitisho vingine vilitokana na ugaidi pamoja na vita vya kulipiza kisasi baina ya makabila katika *Usiku wa Manane* (Kobia 2010)

Uchunguzi wa maudhui katika hadithi ya *Usiku wa Manane* (Kobia 2010) umedhibitisha kuwa mwandishi alinuia kuyaweka wazi mateso yaliyowahi kuwapata wananchi kutokana na ghasia za baada ya uchaguzi mkuu. Katika ghasia hizo watu wengi waliuawa, kuchomewa nyumba zao na kufukuzwa makwao kutokana na chuki za kikabila zilizotokea kwa sababu za kisiasa nchini Kenya mwaka wa 2007 na 2008 (Khaisie,2018). Maudhui ya vita yalibainika kuwa na hatari ya kuogofya watoto wasomaji kwa kuwa vita vilisababisha majeruhi, vifo, nyumba kuchomwa na watu kufukuzwa makwao. Hadithi hizi basi, zinabainika kuwa na upana na usasa wa maudhui ambao unahusishwa na uandishi wenye mielekeo ya kiuhalisia.

Hatimaye, maudhui ya usalama wa kitaifa yalijitokeza kutokana na matukio yaliyotishia usalama wa raia, usalama wa mali na makazi ya watu, usalama wa afya, usalama wa mazingira na usalama katika usafiri. Usalama wa kitaifa ni jambo muhimu katika fasihi ya watoto, watoto wakihusishwa na masuala hayo utotoni watayakuza hata katika utu uzima. Kama ilivyojadiliwa katika uchanganuzi wa hadithi hizi, maudhui ya kisiasa, vita na vitisho vya kuogofya ni masuala yenye uhalisia katika jamii. Waandishi wa hadithi teule huyaweka katika kazi zao ili yasomwe na watoto na kuwafunulia watoto uhalisia wa jamii zao ili wawe tayari kupambana nayo wanapokua.

Matokeo ya utafiti huu basi, yatarekebisha mawazo ya hapo awali kuwa hadithi katika fasihi ya watoto huwa haishughulikii baadhi ya mambo yanayowahusu watu wazima katika jamii Hunt (2002). Hivyo, kinyume na dhana ya fasihi ya watoto iliyo na watu wengi, hadithi za watoto si masimulizi kwa watoto tu kwa ajili ya kuwaburudisha na kuwasaidia kupitisha wakati kwa kuwapa kitu cha kufanya wasikae bure. Ni kazi zilizo na uhusiano mkubwa na maisha ya kila siku ya binadamu hasa zikitazamwa kwa mielekeo ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Hadithi ya *Usiku wa Manane (Kobia 2010)* ilibainika kuwa muhimu kwa maana mtoto angali mtoto na bado anahitaji kuelekezwa kimaadili na kufahamishwa kuhusu mazingira yake kwa kutumia mikakati mahsusi na ya kimakusudi kabla ya kutoswa kwenye ulimwengu wa watu wazima.

Mwandishi Wamitila katika hadithi ya *Kijana Mpelelezi (2007)* anaonesha kijana Kangwana ambaye alipeleleza kuhusu nyumba ya shangazi yake na kugundua kuwa mzee Majungu ndiye aliyekuwa akiendeleza vitisho ili nyumba hiyo kusemwa kuwa ilikuwa na majini. Matokeo haya ya upelelezi yanaambatana na hoja ya Ngugi (2014) akimrejelea Cass (1967) kuwa uadilifu katika hadithi za watoto huhimizwa ili ionekane ya kwamba wema unakwezwa na kushinda uovu. Katika jamii wahusika kama mzee Majungu wapo na huo ni uhalisia.

### 5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanathibitisha kuwa, hadithi za watoto zilizoteuliwa zinawaelimisha watoto na kuwafanya waielewe si jamii yao ya nyumbani tu bali nchi yao

kwa jumla.  Mathalani, hadithi zilizoteuliwa zinawaelimisha watoto kuhusu uchaguzi wa kisiasa.  Jambo hili linaweza kuwapa mwelekeo wanapowachagua viongozi wao shuleni kinyume na miaka ya zamani ambapo viranja shuleni walikuwa wanateuliwa na walimu.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu kuwa vita vya kikabila vilitokea kwa sababu ya watu kukosa kukubaliana na matokeo ya uchaguzi, ni muhimu basi watoto wafundishwe kuhusu upigaji kura wa amani.  Kutokana na mabadiliko ya kiwakati katika baadhi ya shule za msingi uchaguzi wa viranja huchukua mkondo wa uchaguzi wa kisiasa nchini Kenya ikiwemo kusimamiwa na maafisa wa Tume Huru ya uchaguzi na mipaka (IEBC) pale nyanjani.  Maafisa hao huwafunza watoto katika shule hizo namna ya kupiga kura kwa amani, huwaelekeza kupiga kura na hatimaye hutangaza washindi baada ya kura kuhesabiwa ambapo wanafunzi waliofanya uchaguzi hushuhudia.  Kabla ya uchaguzi huo wawania nyadhifa mbalimbali huwa wamepewa muda wa kufanya kampeni ili kutangaza manifesto zao kwa wanafunzi wenzao.  Huandaa mabango na kuyatumia katika kampeni za kujipigia debe.  Shughuli hiyo husifiwa na walimu wao kuwa yenye nia ya kuwaandaa wanafunzi kuwa viongozi waliowajibika katika siku za baadaye.  Ikiwa wanafunzi hao watakuwa wamepata tajiriba kwa kusoma vitabu vya hadithi vinavyoelekeza ifaavyo jinsi ya kufanya uchaguzi wa amani, watakuwa na maarifa kuhusiana na mchakato mzima wa uchaguzi.

Aidha, watatambua umuhimu wa kudumisha amani kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi. Pia, watajenga mitazamo ifaayo kama vile walioshindwa kukubali matokeo na kujiunga na walioshinda kuendeleza shughuli za kila siku za maisha shuleni na katika jamii pana.  Kwa mfano, katika shule moja wanafunzi wa darasa la sita na la saba walikosa kuelewana kuhusu matokeo ya uchaguzi wa viranja shuleni mwao (Tazama kiambatisho C chenye anwani; *Pupils dispute election results at Kericho school*, ‘Daily Nation’ July 25, 2018) wanafunzi hao walitaka kura hizo zihesabiwe tena.  Ni baada ya zoezi la kuhesabu kura kurudiwa ambapo walioshindwa waliridhika na kukubali kuwapongeza walioshinda na kuahidi kuwaunga mkono.

Kutokea kwa mambo haya miongoni mwa watoto wa gredi ya sita wa enzi hii kunaonyesha hali imeanza kubadilika kutokana na mpito wa wakati. Inapendekezwa kuwa inastahili mchakato wa kudumisha amani kupitia kwa fasihi ya watoto kimaudhui uanze kitaaluma kwa lengo la kuibuka na mitazamo mipya kuhusu uhalisia wa kimaudhui unaopatikana katika hadithi za watoto na kwa mapana fasihi wa watoto kwa jumla.

Pendekezo la pili kutokana na mielekeo mipya ya kimaudhui inayobainika kutokana na uchanganuzi wa hadithi katika utafiti huu, inapendekezwa kuwa kozi ya fasihi ya watoto ianzishwe katika vyuo vya walimu wa shule zote za msingi ama vyuo vikuu. Usomaji wa hadithi za watoto katika vyuo vya walimu utawezesha wakurufunzi wanaojifunza ualimu kujifunza uchanganuzi wa hadithi za watoto kimaudhui kwa kuwa zinaelekea kuchukua mielekeo mipya. Hivyo wanafunzi hao wanaojiandaa kuwa walimu watapata fursa ya kujiongezea maarifa kuhusu fasihi ya watoto.

Maarifa ya kutosha kuhusu fasihi ya watoto yatawawezesha kuithamini fasihi hii na hivyo kuthamini usomaji wa hadithi za watoto shuleni. Kufikia wakati wa utafiti huu, pamekuwa na pengo kwa kuwa wakurufunzi hao wakiwa vyuoni walikuwa wakisoma fasihi ya watu wazima ilhali siyo fasihi ambayo wanatarajiwa kufundisha katika shule za msingi. Utafiti huu unapendekeza wasome hadithi za watoto zilizoteuliwa badala ya vitabu vya fasihi ya watu wazima ili kujenga stadi za kufundishia fasihi ya watoto kutokana na umuhimu wake. Usomaji wa hadithi za watoto utawasaidia wakurufunzi hao vyuoni kuwaelewa watoto hata zaidi na kujenga taswira nzuri kuhusu ukuaji wa watoto na jinsi uwezo wao wa kusoma unavyofaa kukuzwa.

Kadhalika kutokana na utafiti huu pendekezo la tatu ni kuwa kusomwa kwa hadithi za watoto shuleni kusiwe kwa kujiburudisha tu lakini kuende hatua zaidi kutilia mkazo usomaji unaojenga mitazamo yenye maadili mema kwa watoto wakiwa bado wadogo kulingana na matukio ya kisiasa katika jamii. Somo hili linafaa kuingizwa katika mitaala vizuri na kuwa na baadhi ya vitabu vya hadithi za watoto vilivyopendekezwa kusomwa. Hii ni kwa sababu baadhi ya mambo ambayo watoto wanahitaji kujua kuhusu mazingira yao huenda yasipatikane kwingineko kwa njia faafu kama katika vitabu wasomavyo.

Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa hadithi za watoto zinaweza zikatumiwa kuelimisha jamii kuhusu athari ya siasa mbaya, vita na chuki za kikabila lakini kwa kutumia mikakati mahususi. Hivyo, inapendekezwa kuwa waandishi wa hadithi za watoto hasa wale wanaoinukia, waelimishwe kupitia kwa semina mbalimbali kuhusu maswala mtambuko yanayoathiri jamii na jinsi ya kuyashughulikia kwa njia fiche kiubunifu katika hadithi za watoto.

Hatimaye kutokana na utafiti huu, panahitajika kuzuka tafiti nyingine. Kwanza utafiti zaidi unahitaji ufanywe kwa kutumia nadharia ya mwitikio wa msomaji kukadiria iwapo watoto wanaweza kutambua maudhui yaliyofichika katika hadithi. Pili, tathmini ya tafiti zilizofanywa kuhusu fasihi ya watoto inaonyesha kuwa tafiti hizo zimejikita zaidi katika utanzu wa hadithi za watoto. Kuna pengo la kiutafiti basi katika tanzu nyingine za fasihi ya watoto. Hatimaye utafiti huu unahusu uhalisia wa maudhui ya usalama yanayohusishwa na watoto katika hadithi teule za fasihi ya watoto. Kuna haja ya kuchunguza ikiwa kuna mielekeo mipya katika hadithi za watoto zilizoandikwa ikilinganishwa na vipindi vingine vya kiwakati. Utafiti wa kutosha katika fasihi ya watoto ni muhimu kwa kuwa utaweza kuendelea kuboresha kazi za fasihi ya watoto za baadaye hasa matokeo ya tafiti hizo yanapochapishwa.

## MAREJELEO


Ahmed, A. H. (2003), *Kifimbo Cha Cheza*. Nairobi: Oxford University Press.
Atieno, W & Ocharo, B. Taifa leo.nation.co.ke. Sept 13th,2021.

Bainbridge, J. (2005). *Canadian Children's Literature*: An Alberta Survey in *Alberta Journal of Educational Research*, 51(4).

Bakari, A. (2008). Ngoma *za Uchawi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Bakize L.H. (2013). *Changamoto Zinazoikabili Fasihi ya Watoto Nchini Tanzania*: Dar-es Salaam.

Bakize, L.H, Ngugi, P.M.Y., & Lyimo, E.B. (2018). *Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto nchini Tanzania na Kenya: Mkabala LinganishiKiswahili*,80(1).

Bekoe, D. (2012) Voting in fear: Electoral violence in sub-saharan Africa.

Bhroin C. & Patricia Kennon (2012). *What Do We Tell the Children? Critical Essay Children's Literature*. Cambridge Scholars publishers.

Bulaya, J., & Mhango, P. (2020). *Ujitokezaji wa Maudhui ya Utunzaji wa Mazingirakatika Hadithi Teule za Watoto*: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili. Mulika Journal,38 (1).

Buliba, A. Mayaka, G. na Riro M. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Education Publishers (T) Ltd.

Cooke,J. WWW.CSIS.org:Post-election violence in Kenya and its aftermarth.August 11th ,2009.

Coser, L. (1963) *Sociology Through Literature* : Prentice-Hall.

*Farsy M (1960), Kurwa na Doto. Dar-es Salaam: East African Literature Bureau*
Gay, L. R., Mills, G. E., & Airasian, P. (2006). *Educational Research: Competencies for Analysis and Applications*. Columbus: Merrill Greenwood.

Government Printer, (2010) *Katiba ya Kenya*: Nairobi.

Haji, M. D. I. (2018). *Uhalisia wa Utabaka katika Tamthilia ya Janga la Werevu na Kitumbua Kimeingia Mchanga* (MA dissertation, The State University of Zanzibar (SUZA).

Herman, L. (2018). *Fantasia Katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto. Kioo cha Lugha*,10(1).

Howe, M (1970) *Using Students' Notes to Examine the Role of the Individual Learner in Acquiring Meaningful Subject Matter*: Linguistics, Psychology Journal of Educational Research.

Hunt, P. (ed) (2002). *Understanding Children's Literature.* Taylor & Francis e-library.

IEBC (2012). Voter Education Training Manual. Nairobi: IEBC.

Jupp, V. (2006). *The Sage Dictionary of Social ResearcMethods*. London: Sage Publishers.

Kairu, W.M. (2005) *Uhalisi na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya watoto*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta (Hiajachapishwa).

Karin, L. (2004). *Children's Literature: New Approaches*. New York: Palgrave Macmillan.

Karoki, E. (2014) *Suala la Uhamaji na Uhamiaji kama Linavyoendelezwa katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani* ya Adam Shafi.

Karuga, M.N. (2005) *Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Kea, P. (2009) *Pupa na Bupa*. Nairobi: Oxford University Press.

Kerlinger, F. N. (1986). *Foundations of Behavioural Research (3rd ed)*. New York: Holt Rinehart and Winston.

Khaisie, J.L.W (2018 *Matumizi ya mikakati ya Propaganda katika Mdahalo wa Urais wa Kenya wa Mwaka wa 2013. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Laikipia* (Haijachapishwa).

Kisovi, C. (2005) Mama *wa Kambo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Kobia, J. (2008). Siku *ya Ukimwi*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Kobia J. (2010), Usiku *wa Manane*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kothari, C.R. & Gaurav G. (2014). *Research Methodology: Methods and Techniques 3rd Edition*. New Delhi: New Age International Publishers.

Manji, A (1996) *Bonde La Wafu*. Nairobi: Phoenix.

Mailu, G. (1997*) Atendaye Mema*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Publisher.

Matundura (2005). Mwepesi *wa Kusahau*. Nairobi: Phoenix.

Matundura (2007), *Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Matundura (2014), Likizo *ya Mkosi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Maniza, z. (2022) *General elections-why children matter*. Unicef.

Mdari, A. (2001). Yalianza *Kimchezomchezo*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Michuki, D (1969*) Kaka Sungura na Wenzake*, Nelson Publisher. Nairobi.

Miricho, E.M. (2015), *Usawiri wa Watoto katika Hadithi za "Mwepesi wa Kusahau" na "Likizo ya Mkosi*". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Miricho ,E.M (2021), Ukiushi *wa Kanoni Katika Hadithi Teule za Watoto za John Kobia na Wadi Wamitila*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu (Haijachapishwa).

Ministry of Education (2015) *Approved List of School Textbooks and Other instructional materials for primary schools.* Nairobi.

Mkufya, W. (1998) *Androko na Simba.*Tanzania: Mwanzo Educational Publisher.

Mogambi, H. (2014), *Usilie, Yakobo*. Nairobi: Phoenix.

Mpesha, N. (1991*), Nyani Mdogo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mpesha, N (1996), *Children's Literature in Tanzania. A Literature appreciation of Its growth and development*. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Muhammad, S (1974*) Siri Ya Sifuri,* Nairobi: East African Publishing House.

Muhammad, S. (1968*) Kisima Cha Ginigi*, Nairobi: Evans Brothers.

Muhammad, S. (1977) *Mzimu Wa Watu Wa Kale*, Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Muriungi, C.K. (2014) *Transformations in Children's Prose Fiction in: Journal of arts and Humanities*, (JAH) Volume 3, No. 4.

Muthubi, F. (2005). *Mikakati na Mbinu za Usilimishwaji Katika Fasihi ya Watoto.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwangi, J. W. (2013). *Uhalisia na Uhalisiajabu katika riwaya mpya*: *Babu Alipofufuka* (Said Ahmed Mohamed) na *Watu wa Gehenna* (Tom Olali) (Masters dissertation, University of Nairobi).

Nandwa, R. (2006), *Nampenda Mama wa Kambo*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ngugi, P.M. (2003), *Nikicheka Anacheka*. Nairobi: Oxford University Press.

Ngugi P.M (2005), *Ujeuri wa Mbwa*. Nairobi: Phoenix.

Ngugi P.M (2006), *Alipata Tuzo*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Ngugi P.M (2009), *The State of Children Literature in Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Vienna. Austria.

Ngugi P.M (2014), *Fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji ya mtoto kisaikolojia Katika Kiswahili* Journal of the Institute of Kiswahili Studies Vol. 77 (TATAKI). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kur 170-180.

Ngugi P.M (2016). *Usawiri wa Masuala Ibuka katika Fasihi ya Watoto*: Mifano kutoka Kenya katika: Mulika, No. 35. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur. 76 – 86.

Njogu, K. na Chimerah, R (1999), *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyaga, F.M (2017). *Itikadi za Kisiasa katika Vitabu Teule vya Fasihi ya watoto ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Cha Chuka. (Haijachapishwa).

Omolo, L (1971) *Tajiri Mjanja*. Nairobi: East African Publishing House.

Osman, S.A., Yan, L.s., & Kassim, S.R. (2017). *Recent trends and themes in Malaysian children's fiction*. In The Routledge Companion to International Children's Literature (pp.410420). Routledge.

Reynolds, K. (2007) *Radical Children's Literature*. New York: Palgrave Macmillan.

Shaaban, R (1952) *Adili na Nduguze*, London: New York; Macmillan Education.

Sutherland, R. (1985). *Hidden Persuaders: Political Ideologies in Literature for Children*. In Children's Literature in Education, Vol. 16 No.3: Agathon Press, Inc.

Swingerwood A. 1975 *The novel and Revolution*. London: The Macmillan Press Ltd.

Wafula Na Njogu (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walliman, N (2001). *Your Research Project*. London: Sage Publishers.

Walibora, K. (2001). *Ndoto ya Amerika*. Nairobi: Sasa Sema (longhorn).

Wamitila K.W (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila K.W (2006). *Uhakiki wa Fasihi*: Nairobi Phoenix.

Wamitila K.W (2007*). Kijana Mpelelezi*, Nairobi: Vide – Muwa Publishers.

Wamitila K.W (2008). *Kanzi ya Fasihi*: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi Nairobi: Vide-muwa Publishers.

Wamitila K.W (2013). *Kesi ya Kuchekesha*. Nairobi: Vide – Muwa Publishers.

Warren na Wellek (1973). *Theory of Literature*. London: Penguin Books.

Waiyaki,W &Onyango, M (2017) *Kenya's Post election violence: the harm that's been done to children*. Daystar University Published: August,17,2017.

## VIAMBATISHO

**Kiambatisho A: A childs exposure to violence can lead to lasting physical, mental and emotional harm. Georgina Cranston/Reuters**





**Kiambatisho B: Watoto Kuangamia Katika Vurugu Baada Ya Uchaguzi Mkuu. (Stephanie Moraa kutoka Mathare, Nairobi na Baby Samantha Pendo Kutoka Kisumu)**



**Kiambatisho C: Daily Nation July 25, 2018**



# Pupils dispute election results at Kericho school

BY ANITA CHEPKOECH

[illegible]

**182**

**140**

**Kiambatisho D: Utaratibu wa kazi**

| SHUGHULI | WAKATI |
|---|---|
| Uandishi wa pendekezo la utafiti | Aprili 2020 – Juni 2020 |
| Uwasilishaji katika idara | Mei 2021 |
| Uwasilishaji katika kitivo | Juni 2021 |
| Utafiti, uandishi wa tasnifu pamoja na uwasilishaji katika ngazi mbalimbali | Agosti 2021 – Disemba 2022 |
| Uchapishaji wa Makala | Disemba 2022-Machi 2023 |
| Mahafali | 2023 |

**Kiambatisho E: Makadirio ya gharama ya utafiti**

| | |
|---|---|
| Ununuzi wa vifaa vya kufanya utafiti na kuandalia pendekezo la tasnifu.<br><br>Utafutaji wa mapitio ,ununuzi wa vitabu na majarida | 30,000.<br><br><br>20,000 |
| Ukusanyaji na uchanganuzi wa data.<br><br>Huduma ya mitandao<br><br><br>Uwasilishaji wa taarifa na uandalizi wa makala.<br><br>Kuchapisha makala matatu.<br><br>Kuhudhuria na kuwasilisha katika makongamano matatu.<br><br>Mchakato wa utoaji nakala baada ya kupiga chapa | 30,000<br><br>20,000<br><br><br>10,000<br><br>10,000<br><br>20,000<br><br><br>5,000 |
| Usafiri<br><br>Simu<br><br>Matumizi madogomadogo | 5000<br><br>3,000<br><br>10,000 |
| JUMLA | 168,000 |